BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,016,428,582/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 2

**Ajira** mpya 740 zatangazwa na OR - TAMISEMI




UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Julai 21, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581013

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Mitihani 11 IGP mpya



Samia atangaza mabadiliko makubwa vyombo vya ulinzi na usalama, kamati uchunguzi yaundwa rasmi... Uk. 2 & 4

Rais Samia Suluhu Hassan, akimvalisha cheo kipya cha Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi (IGP), aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camillus Mwongoso Wambura kuwa Mkuu mpya wa Jeshi hilo, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## CCM yashtuka tishio la njaa

UKURASA 2

UKURASA WA 3



### MOI YAREJESHA MATIBABU WATU WALIOPOTEZA VIUNGO

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), imeanza kutengeneza viungo bandia kwa kutumia mfumo...

UKURASA WA 7

### NDALICHAKO AANZA KUSIKILIZA KERO MAFAO YA WASTAAFU

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amejipanga kupiga kambi kwenye mikoa...

UKURASA WA 7



### MAGARI YALIYOTUMIKA KUKAGULIWA JAPAN KABLA KUINGIA TZ

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema kuanzia Julai 20, mwaka huu magari yote yaliyotumika yanayotoka nchini Japan yatakuwa yanakaguliwa nchini humo kabla ya kuja Tanzania kwa utaratibu wa uthibitishaji...

## Serikali yatangaza tathmini ya Katiba

UKURASA 3

**MICHEZO** | MANZOKI AIKAMUA SIMBA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Rais Samia atangaza mabadiliko makubwa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema amefanya mabadiliko madogo ndani ya Jeshi la Polisi huku akisisitiza yatafuatwa na mabadiliko makubwa.

Amesema kutafanyika maboresho na mageuzi kwenye taasisi za haki jamii inayojumuisha jeshi hilo, Ofisi ya Mashtaka, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Jeshi la Magereza na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Pia amesema watatazama upatikanaji wa watendaji kazi kwenye majeshi na hata kama yalishapita, huko mbele watachujana ili kuyajenga majeshi kuwa na sifa na hadhi ya kusimamia nchi.

Rais Samia aliweka bayana mpango huo jana Ikulu mkoani Dodoma wakati akimwapisha Mkuu wa Jeshi la Polisi mpya, IGP Camillus Wambura na mabalozi aliowateua.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Samia alisema IGP Simon Sirro ambaye sasa anakwenda kuwa Balozi wa Tanzania huko Zimbabwe, amelitumikia Jeshi la Polisi kwa muda wote na kulisogeza na wameshuhudia maendeleo mengi lakini wanakokwenda, mabadiliko ni lazima.

"Imenipendeza kama Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi kufanya mabadiliko kidogo ndani ya Jeshi la Polisi na pengine baadaye yatafuatiwa na mabadiliko makubwa, lakini tumeanza hapa.

"Pamoja na kukushukuru, nikupongeze kwa kuwa sasa ukatusaidie pale Zimbabwe hutakuwa mbali na nyumbani, sera zao na zetu zinafanana, wanahitaji mtu wa aina yako," alisema.



Rais Samia alimpongeza IGP Wambura kwa kazi nzuri aliyofanya ndani ya Jeshi la Polisi kwa muda wote na kupata imani hiyo ya kukabidhiwa chombo hicho.

"Wewe ndiye IGP na Mkuu wa Jeshi la Polisi, ninachotegemea kutoka kwako ni mabadiliko makubwa ndani ya Jeshi la Polisi, kuona ufanisi ndani ya Jeshi la Polisi, kuona usalama wa raia na mali zao unaimarika ndani ya Jeshi la Polisi.

"Tutakwenda kuyaongea baadaye lakini ninakupongeza kwa kazi nzuri na ninakushukuru uliyofanya nyuma kama mwanajeshi la polisi kama DCI, ninakupongeza kwa wadhifa huu mpya uliopata leo," alisema.

**KAMATI YAUNDWA**

Rais Samia alitangaza kuunda kamati ya watu 12 na sekretarieti ya watu watano kwa ajili ya kufuatilia utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini.

Alisema kamati hiyo itaongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othumani Chande na makamu wake atakuwa aliyewahi kuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Ombeni Sefue, akisisitiza kuwa itakuwa ikimshauri njia bora ya kuleta mabadiliko ya utendaji kazi wenye matokeo bora kwenye vyombo vya haki jinai.

Alisema kamati hiyo itaanza na polisi na ikishamaliza huko, itamsaidia kufanya marekebisho na baadaye watakwenda kwa majeshi mengine mpaka wamalize.

Alisema serikali kwa sasa inakwenda na jicho la ulinzi kwa majeshi hayo na kamati hiyo kila ikimaliza kulichunguza jeshi, itampelekea mrejesho ili kujenga majeshi imara na bora.

**ACT-WAZALENDO**

Baada ya Rais kutangaza kuunda kamati hiyo, Chama cha ACT Wazalendo kilisema kuna haja iwe shirikishi zaidi kwa wadau wote wanaoguswa na huduma ya Jeshi la Polisi.

Msemaji wa Sekta ya Mambo ya Ndani wa chama hicho, Maharagande Mbarala, alisema: "Tunatoa wito kwa serikali kuongeza wigo wa timu hii kwa kuhusisha wadau wengine ili kulifanya Jeshi la Polisi kuakisi matarajio na matamanio ya watu wanaowahudumia."

Rais Samia katika uteuzi wake huo, amempandisha cheo Kamishna wa Polisi Wambura kutoka DCI kuwa Inspekta Jenerali na Mkuu wa Jeshi la Polisi. Pia amempandisha cheo Kamishna Msaidizi wa Polisi Ramadhan Kingai kuwa kuwa DCI.

## TAMISEMI yatangaza ajira 746 kada ya afya

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetangaza tena ajira za watumishi 746 wa kada mbalimbali za afya ambazo zilikosa waombaji wenye sifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, ajira hizo ni kwa ajili ya hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati zilizo chini ya mamlaka za serikali za mitaa.

Alisema tangazo hilo linarudiwa kwa mara ya pili baada ya kukosa waombaji wenye sifa katika tangazo la awali lililotolewa Aprili 20, mwaka huu.

Prof. Shemdoe alitaja nafasi zinazotangazwa ambazo idadi yake iko kwenye mabano ni madaktari wa meno daraja la pili (30), matabibu meno daraja la pili (43), matabibu wasaidizi (244), maofisa teknolojia (maabara) daraja la pili (30), wateknolojia (mionzi) daraja la pili (86) na wauguzi daraja la pili (313).

Aliwataka waombaji kuzingatia vigezo vilivyotolewa kwenye ajira hizo na maombi hayo yatafanyika kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ajira. tamisemi.go.tz.

"Waombaji wenye ulemavu na sifa zilizoainishwa katika tangazo hili watume maombi yao ya kazi kwa nakala ngumu maombi yao yaeleze aina ya ulemavu wao," alisema na kubainisha kuwa mwisho wa maombi hayo ni Agosti 2, mwaka huu.

Aprili, mwaka huu, ofisi hiyo ilipata kibali cha kuajiri walimu 9,800 wa shule za msingi na sekondari, na wataalamu wa afya 7,612.

STEP MARK

Makumbusho, PLOT No. 13 Block 45, P.O.Box 11767, Dar es salaam, Tanzania
Office : +255 715 300 312 , E-mail: info@stepmark.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA!!

Step mark Limited kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya CRDB Makao Makuu yaliopo Plot Namba. 25&26 Ally Hassan Mwinyi Road & Plot Namba.21. Barack Obama Road, S.L.P 268,11101 Dar es Salaam** tunatangaza minada ya hadhara wa kuuza mali za wadaiwa wa **Benki ya CRDB** sehemu mbali mbali katika mikoa ya Tanzania.

Mali hizo zitauzwa kama zilivyo kwenye eneo kwa njia ya Minada ya hadhara..

| S/No | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI | TAARIFA YA MALI INAYOUZWA | ENEO MALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Israel Delius Mahenge | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa: Mwanyanje Kata: Igawilo Jiji la Mbeya. | 09/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 2. | Clement Said Sangale | NYUMBA | Hati namba: 9069-MBYLR Namba ya makazi:178947 | Ploti namba:53 Block 'C' Mafinga Urban | 06/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 3. | Joshia Daniel Magabe | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa; Mponja Kata;Igawilo Jiji la Mbeya | 12/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 4. | Emil Augustino Mzumbwe | SHAMBA | Hati namba; 9570-MBYLR Namba ya makazi;228486 | Namba ya shamba 854 Kijiji:Isansa Wilaya:Mbozi | 09/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 5. | Emil Augustino Mzumbwe | SHAMBA | Hati namba; 9572-MBYLR Namba ya makazi;228483 | Namba ya shamba 853 Kijiji:Isansa Wilaya:Mbozi | 11/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 6. | Samwel Jacob Masasi | NYUMBA | Hati namba: 30492-MBYLR Namba ya makazi:502170 | Ploti namba:477 Block 'A' Mafinga Urban | 09/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 7. | Barusha Matondane Masanja | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Ploti namba 63 (a) Block 'DD' Mtaa;Bondeni Kyela Urban | 14/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 8. | Esikaka Karibu Mahenge | NYUMBA | Hati namba; 24559-MBYLR Namba ya makazi;189717 | Ploti namba:544 Block 'C' Kalumbulu, Kyela Urban | 16/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 9. | Ivod G. Chalula | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kalalasi,Wilaya ya Kalambo Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 12/08/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 10. | Apolinary Sipliano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji cha Ninga,Wilaya ya Kalambo Mkoa wa | 14/08/2022 Saa Nne |
| 11. | Apolinary Sipliano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji cha Ninga,Wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa | 14/08/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 12. | Gasper Johnson Kiondo | NYUMBA | Hati Namba 89-RKLR Ofisi ya Ardhi Namba 791609 | Plot Namba 383, Block "T" Eneo la Kisiwani,Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 16/08/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 13. | Venus joseph ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; minsukumilo Kata;kipindu Wilaya; Namanyere Mkoa;sumbawanga | 18/08/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 14. | Venus Joseph Ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; sheli Kata; Nchola Wilaya; Namanyere Mkoa;Sumbawanga | 20/08/ 2022 Saa Nne Asubui Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 15. | Alfred Sanga | NYUMBA | Hati Namba 10718-MBYLR Ofisi ya Ardhi Namba 174787 | Ploti namba: 112 BLOCK "P" Tukuyu | 27/08/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi lazima afike eneo la mnada unapofanyika
2. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano(25%) ya bei iliofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano(75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya mnada na mteja akishindwa kulipa 75% ndani ya siku 14 atakua amepoteza haki ya ununuzi.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA 0677 992 040 /0677 992 030**

116954101

## CCM yashtuka tishio la njaa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeelezea wasiwasi wa kuwapo kwa baa la njaa nchini kutokana na mwenendo wa mavuno pamoja na biashara ya nafaka nje ya nchi.

Kutokana na hali hiyo, Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, ameiomba serikali kuanzisha utaratibu wa kuhifadhi chakula ili kukabiliana na hali hiyo hapo baadaye.

Alibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, January Mkamba, mkoani Shinyanga, alipopita kwenye ofisi za CCM kuzungumza na viongozi wa chama na kutia saini kitabu.

Magesa alisema sasa hivi kuna malori kutoka Uganda na Kenya yanaingia nchini na kusomba vyakula vingi na kupeleka nchini kwao, hali ambayo ni ishara mbaya kuwa kutakuja kutokea baa la njaa hapa nchini, na kuiomba Serikali ianze taratibu za kuhifadhi chakula ili kukabiliana na tatizo hilo siku zijazo.

"Tunakuomba Waziri utufikishie salamu zetu huko juu kuwa serikali ianze taratibu za kuhifadhi chakula sababu hapo baadaye kunaweza tokea baa la njaa, Kenya na Uganda wanasomba sana chakula na kupeleka nchini kwao na huwezi kutawala vizuri kama watu wana njaa,"alisema Magesa.

Katika hatua nyingine, aliomba suala la kupanda kwa gharama za kunganishiwa umeme kutoka Sh. 27,000 hadi 320,000 liangaliwe vizuri kwa sababu wananchi wamekuwa wakiwahoji maswali kuwa waliwadanganya kwenye uchaguzi mkuu ili wapate kura na wamekiuka ilani yao.

Waziri Makamba, alisema suala la kuhifadhi chakula atalifikisha sehemu husika, na kutolea ufafanuzi kupanda kwa gharama za kuunganishiwa umeme kuwa sasa hivi kuna timu inapita kuona watu gani wanapaswa kulipa gharama hiyo ya Sh. 27,000.

"Kupanda kwa gharama hizi za kuunganishiwa umeme kutoka Sh, 27,000 hadi 320,000 ni kweli limeleta mtihani. Ila sasa hivi kuna timu ya wataalamu inapita kutazama watu gani wanastahili kulipa gharama hiyo ya Sh. 27,000 kuunganishiwa umeme na ikikamilisha tutatoa muongozo," alisema Makamba.

Pia alisema kuna watu wengine wana uwezo mkubwa na wana maeneo ya biashara, hivyo hawawezi kuunganishiwa umeme kwa bei hiyo ya Sh.27,000 ndiyo maana ilibidi wabadilishe gharama hizo, ili serikali ipate fedha za kufanyia matengenezo vifaa vyake na kutoa huduma stahiki ya umeme kwa wananchi.

# Serikali yatangaza tathmini ya Katiba

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema katika mwaka huu wa fedha 2022/23, wataalamu watafanya tathmini ya katiba ili watu waseme mazuri na mabaya yaliyomo yatakayowezesha kupata katiba ambayo itadumu muda mrefu.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, akiainisha mambo makubwa 12 ambayo wizara hiyo imeyapa kipaumbele.

Dk. Ndumbaro alisema ndani ya mwaka huu wa fedha, watatoa tangazo kuziomba asasi ambazo zipo tayari kusaidia kutoa elimu kuhusu katiba kwa wananchi.

Alisema mjadala uliopo kwa sasa ni upatikanaji wa katiba ya tano ambayo serikali inataka ipatikane iliyo nzuri zaidi na siyo baada ya muda mfupi waanze tena mchakato mwingine wa kutaka katiba ya sita.

"Umesema kwa nini tusitumie rasimu? Unajua Kamati ya Jaji (Joseph) Warioba ilifanya kazi mwaka gani? Kuanzia mwaka 2012 mpaka leo ni miaka mingapi? Mtu aliyekuwa na miaka minane wakati ule, leo ana miaka mingapi? alishiriki mchakato wakati ule? Hakushiriki.

"Ukienda RITA (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) watakwambia hao ni wengi kweli. Je, tusiwasikilize hao? Kuwa na umri mkubwa siyo kwamba una akili zaidi, vijana hawa wapo wenye mawazo ya maana na wengine wameshakuwa viongozi wa vyama, taasisi na wasomi, tusiwasikilize? Kingine ni muda, miaka 10 ni mirefu sana? Mabadiliko yaliyofanywa ni mengi.

"Hivi kule bungeni rasimu iliishaje, ilifikia mwafaka? Ile katiba pendekezwa bungeni kulikuwa na mwafaka? Watu si waligawana kuni kule, UKAWA walitokea huku CCM walitokea kule, kulikuwa na maridhiano? Kama kati ya wanasiasa hakukuwa na maridhiano na hili ndo kundi moja la watawala, je, kundi la wananchi?" alihoji kwa msingi kwamba kuna haja mchakato wa Katiba Mpya unatakiwa kuanza upya na siyo kuendeleza ulipoishia.

Waziri Ndumbaro alisema haipondi rasimu wala katiba pendekezwa lakini kama ni nzuri, zirudishwe kwa wananchi ili kizazi kipya kitoe maoni.

Alisema katiba imeandikwa na wanadamu, hivyo ni lazima ina upungufu ingawa hilo halina maana yote ni taka.

"Lakini, haimaanishi katiba ya mwaka 1977 imepitwa na wakati, yapo mazuri. Moja kati ya mazuri ni Machi 17, 2021, kwa mara ya kwanza tulipoteza Rais aliyekuwa madarakani, Hayati John Magufuli, haijawahi kutokea katika nchi hii, kuugua kwa Rais ni hoja ya kikatiba, Rais asipoonekana hadharani ikapita wiki mbili mnaanza kuuliza.

"Kifo cha Rais ni jambo kubwa la kikatiba dunia nzima ilituangalia je, Tanzania itatoka? Tuliwaambia kwamba jibu letu ni katiba, ingekuwa mbaya hili lingetuvusha? Tungesema tuandike katiba mpya tuondoe hilo. Kwa hiyo, yapo mazuri yaliyopo katika katiba ya sasa," alisema.

Waziri Ndumbaro alisema ndiyo maana wameamua wataalamu ndani ya mwaka huu wafanye tathmini ili watoe elimu kwa kuyasema mazuri na mabaya.

"Kwanini? Ili wananchi wauone huu mkataba wao, wauelewe mkataba wao, tuelimishe wananchi katika mkataba huu wapi ni pazuri, wapi ni pabaya.

"Shida ninayoiona kwenye mjadala unaoendelea tunaoongea ni sisi wanasiasa, tunaoongea ni sisi vyama vya siasa, ni vizuri tuwasikilize wananchi kwa sababu wanasiasa na vyama vya siasa wote ni kundi moja, hawa ni watawala kama siyo wa leo basi kesho," alifafanua.

# MOI yarejesha matibabu watu waliopoteza viungo

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), imeanza kutengeneza viungo bandia kwa kutumia mfumo wa umeme.

Tangu kuanza kwa huduma hiyo nchini Mei, mwaka huu, tayari wagonjwa watatu wamewekewa mikono bandia ya mfumo wa umeme inayowasaidia kukunja mikono, kunywa maji na kukamata vitu.

Mkuu wa Kitengo cha Maabara ya Viungo Bandia na Vifaa Saidizi wa MOI, Dk. Godfrey Mwakasungula, akizungumza na Nipashe jana, alisema mkono huo unaunganishwa na umeme na misuli ya mwili wa binadamu ili kumsaidia na kumpa urahisi wa kufanya shughuli zake kama ilivyokuwa awali.

Alisema mkono huo unakuwa na 'terminal' mbili ambazo moja inaunganishwa kwenye msuli ambao unasaidia kuunyoosha, kukunja au kukamata.

"Unaweza kukamata chupa ya maji, ukainyanyua na ukanywa bila shida yoyote kwa sababu mkono huo unakuwa umeunganishwa kwenye msuli wa mkono ambao unampa urahisi wa kukunja au kukunjua," alisema Dk. Mwakasungula.

Alisema pia umeme unaounganishwa kwenye msuli una uwezo wa kusaidia kiwiko cha mkono kukunja na kukunjuka bila shida yoyote kupitia misuli ya mkono.

Mtaalamu huyo aliwataka Watanzania wenye uhitaji wa vifaa saidizi wafike MOI kwa sababu wanatoa huduma hizo na wameboresha zaidi kwa kuja na vifaa saidizi vyenye kuunganishwa na umeme kwenye misuli.

Alisema awali walikuwa wakitengeneza vifaa saidizi vya mikono na miguu ambavyo haviunganishwi na umeme lakini sasa wanatoa huduma hiyo.

Naye Ofisa wa Viungo Tiba Saidizi na Viungo Bandia wa MOI, Joyce Varisango, alileleza Nipashe kuwa vifaa vya kutengeneza viungo hivyo vinaagizwa kutoka Ujerumani na China.

Alisema vifaa hivyo vikiwasili huanza kumpima mgonjwa kupata ulinganifu wa mkono wake na kungo anachowekewa.

"Kazi ya kuanza kuviunda inachukua hadi wiki mbili na baada ya hapo mgonjwa anakuja kuwekewa kiungo saidizi kwa ajili ya kuendelea na majukumu yake," alisema.

Aliendelea kueleza kuwa, walianza kutoa huduma hiyo Mei mwaka huu, baada ya kupokea oda ya wagonjwa wanaohitaji.

"Tuliagiza mikono bandia na baada ya kuja tukapata mafunzo kwanza kwa sababu ni mara yetu ya kwanza kutoa huduma hii nchini na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu wagonjwa wetu tumeshawawekea na wanaendelea na shughuli zao," alisema Joyce.


**Air Tanzania**
*The Wings of Kilimanjaro*

## VACANCIES ANNOUNCEMENT -READVERTISED

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is making reforms in its structure, internal operations and staffing to accommodate business needs. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the position mentioned below (Previous applicants may re-apply).

**1. POSITION: SENIOR INTERNAL AUDITOR (1 POST)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

* Must have a Bachelor Degree or Advanced Diploma in Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from recognized institutions and;
* CPA (T), ACCA, ACA, CIA or equivalent professional qualification recognized by the NBAA;
* Must have working experience of at least seven (7) years in related field
* Possession of prior aviation experience will be an added advantage

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

* Prepare and arrange for contact with client and execute all required meetings for the allocated audit engagement.
* Review audit tentative programs, internal control and risks and engagement plan
* Administer and coordinate activities of the allocated audit engagement
* Evaluate the adequacy and effectiveness of the controls in the audited areas
* Develop comprehensive practical programs and schedules for Audit Coverage Areas.
* Review all documented audit findings and ensure their effective communication to the client and obtain responses
* Prepare draft and final audit engagement reports
* Schedule project and staff assignment to comply with management needs with scope of the department over all schedules
* Conducts special investigations as assigned by Chief Internal Auditor/ other relevant authorities
* Coordinate Audit schedules to avoid conflict with the external Auditors work
* Assists in the preparation of annual budget and Annual internal audit plan for the unit
* Performs any other duties as may be assigned by superiors.

**2. POSITION : INTERNAL AUDITOR II (1 POST)**

**2.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:**

* Must have a Bachelor Degree or Advanced Diploma in one of the following fields; Auditing Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or Finance or equivalent qualifications from recognized institutions
* CPA (T), ACCA, ACA, CIA or equivalent professional qualification recognized by the NBAA.

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**

* Identify and review all required information and document all controls and risks for internal audit planning
* Develops and execute audit programs as assigned by assignment team leaders
* Conducts audit to appraise the adequacy and use of financial, accounting and operating controls on each assigned engagement
* Conducts special investigations as assigned by Chief Internal Auditor/ other relevant authorities
* Prepares audit reports
* Document all audit working papers as per laid down guidelines on every audit engagement in the permanent and current files
* Participate on preparation of Annual Internal Audit plan
* Follow up on Audit recommendations
* Assists in the preparation of annual budget for the unit
* Performs any other duties as may be assigned by supervisor.

**3. REMUNERATION:**

Attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Scale and Incentive Scheme.

Five (5) years contract.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note:** Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences

**5. CLOSING DATES:**

Applications shall be received within fourteen (14) days from the first date of this announcement and directed to the following address: -

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on 21st July, 2022**

**Welcomes you, to where you can Fly**

# Mitihani 11 inayomkabili IGP mpya

**Na Romana Mallya**

KATIKA kupanga safu za uongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama, Rais Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi mpya katika Jeshi la Polisi huku akimteua Kamishna (CP) Camillus Wambura, kuwa mkuu wa jeshi hilo.




Sambamba na kuteuliwa kushika cheo hicho cha juu katika jeshi hilo, Rais Samia pia alimpandisha Wambura kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) ambacho ni cheo cha juu kabisa ndani ya chombo hicho chenye dhamana ya usalama wa raia na mali zao.

IGP Wambura ambaye ni msomi wa taaluma ya sheria kachero mbobezi ndani ya jeshi hilo, anachukua nafasi ya IGP Simon Sirro ambaye ameteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe.

Wambura ambaye aliapishwa jana Ikulu Chamwino kushika wadhifa huo, anakabiliwa na mambo au mitihani 11 katika uongozi wake ambayo yamekuwa yakionekana kama ni kipimo kwa jeshi hilo katika utendaji wake. Mambo hayo ni;-

### VIFO VYA MAHABUSU

Hili ni jambo ambalo limekuwa likizungumzwa mara kwa mara na hata kulipaka tope Jeshi la Polisi. Kumekuwa na madai ya mara kwa mara kuwa baadhi ya mahabusu wamekuwa wakifariki dunia wakiwa vituo vya polisi kutokana na vipigo kutoka kwa baadhi ya askari.

Agosti 25, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan katika kikao na maofisa wa polisi kwenye Bwalo la Maofisa wa Polisi Oysterbay, Dar es Salaam, alionya kwa marejeo ya kina kuhusu madhila, hata vifo vya watuhumiwa mikononi mwa polisi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) katika ripoti yake ya mwaka 2020, kilibainisha mwaka huo ulikuwa na matukio ya utesaji na kutendwa isivyo halali kati ya raia na vyombo vya dola.

Aidha, Juni mwaka huu, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) katika uchunguzi wake, imebaini kupigwa na kuteswa kwa watuhumiwa wakati wa ukamataji au wakati wa upelelezi kwa madhumuni ya Jeshi la Polisi kupata taarifa zinazohusu matukio ya uhalifu.

Kutokana na kuwapo kwa madai na malalamiko kutoka kwa wananchi ambao ndugu zao wanafanyiwa vitendo hivyo, Rais Samia alilitaka jeshi hilo kujitafakari juu ya utendaji wake.

### KUBAMBIKA KESI

Madai ya polisi kuwabambikia kesi wananchi ni mtihani mwingine unaomkabili IGP Wambura kama ilivyo kwa vifo vya mahabusu katika vituo vya polisi ambavyo vimekuwa vikidaiwa kusababishwa na baadhi ya askari kutokana na vipigo na utesaji dhidi ya watuhumiwa.

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu dhidi ya jeshi hilo kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakibambikiwa kesi zikiwamo za uhujumu uchumi, ugaidi na mauaji.

Jambo hilo pia limekuwa likileta taswira hasi kwa jeshi la polisi kwamba limepoteza mwelekeo na weledi katika kutekeleza wajibu wake. Jambo hilo lilinyoonyeshewa kidole mara kadhaa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli pamoja Rais wa sasa.

### POLISI NA UNYANG'ANYI

Madai ya baadhi ya askari kushiriki katika matukio ya ujambazi na unyang'anyi ni mtihani mwingine ambao utamfanya IGP Wambura akune kichwa katika kuhakikisha anarejesha heshima ya jeshi hilo.

Katika suala hilo, baadhi ya askari polisi wanatuhumiwa kushirikiana na wahalifu kutekeleza vitendo vya unyang'anyi na uporaji na kuchukua mali za wananchi wanaovamiwa, huku miongoni mwao wakifikishwa mahakamani kwa mashtaka ya aina hiyo.

Kama ilivyo katika vifo vya mahabusu na ubambikaji kesi, Wambura na timu yake wana mtihani mkubwa kuhakikisha dhana hiyo inaondoka kwa kufanya mageuzi na hata kulisafisha jeshi kwa kuwashughulikia askari wasio waaminifu.

### PANYA ROAD

Katika siku za karibuni, kumeibuka vikundi vya kihalifu ambavyo vimekuwa vikivamia watu katika makazi yao au wawapo barabarani na kuwapora, kuwajeruhi na hata kusababisha mauaji dhidi ya raia.

Vikundi hivyo, maarufu kama Panya Road, Watoto wa Ibilisi na Tukale Wapi vimekuwa tishio kwa wananchi na mali zao, hivyo uongozi mpya chini ya Wambura una kazi kubwa ya kuhakikisha vinatoweshwa au kusambaratishwa.

### AJALI ZA BARABARANI

Hili ni tatizo sugu kama donda ndugu kwa sasa hapa nchini kutokana na kila uchao kugharimu maisha ya wananchi kutokana na sababu mbalimbali kama vile uzembe wa maderava, ubovu wa magari na mwendo kasi.

Sababu nyingine inayoelezwa kuwa ni chanzo cha ajali ni kukosekana kwa weledi kwa baadhi ya askari hasa wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kuruhusu magari kutembea kwa mwendokasi.

Kutokana na ukweli huo, uongozi mpya chini ya Wambura una kibarua au mtihani mkubwa wa kudhibiti na kupunguza tatizo hilo kama si kumaliza kabisa ili kuokoa nguvu kazi ya taifa ambayo imekuwa ikiteketea kutokana na ajali za barabarani.

### RUSHWA

Moja ya mambo ambayo yanaharibu taswira nzuri ya Jeshi la Polisi ni madai ya rushwa kwa baadhi ya maofisa na askari polisi. Vitendo hivyo vimekuwa vikidaiwa kufanywa na baadhi ya maofisa na askari katika ngazi tofauti ikiwamo kuharibu upelelezi wa kesi au ushahidi.

Pia vitendo hivyo vinadaiwa kushamiri kwa baadhi ya askari wa usalama barabarani. Baadhi ya askari hao wamekuwa wakidaiwa kujihusisha na rushwa ama kwa tamaa zao au kudaiwa kutumwa na mabosi kukusanya 'ushuru' kutoka kwa madereva.

Kazi kubwa inayomkabili Wambura na timu yake atakayoisuka ni kuhakikisha 'kansa' hiyo inatokomezwa na kurejesha heshima kwa chombo hicho hatimaye kurejesha imani kwa wananchi.

### UKATILI WA KIJINSIA

Kumekuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia ya watu kuuawa huku sababu mbalimbali zikitajwa na katika ripoti hiyo ya WHO, ukatili huo unashika nafasi ya 19.

Kuna kazi kubwa ya kuhakikisha tatizo hilo linatafutiwa ufumbuzi wa kudumu kwa Jeshi la Polisi kushirikiana na wadau wengine.

Moja ya mambo yanayopaswa kufanywa ni kuimarisha madawati ya jinsia katika Jeshi la Polisi ili wahusika wa vitendo hivyo washughulikiwe ipasavyo kwa mujibu wa taratibu na sheria.

### DEMOKRASIA

Katika miaka mitano iliyopita suala la mtazamo mpya wa kisiasa, Rais Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake , Jeshi la Polisi lilikuwa likilalamikiwa kuhusika kupiga marufuku mikutano ya kisiasa kwa kuzuia vyama vya siasa kutekeleza wajibu wao wa kidemokrasia.

Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa ni kuwapo kwa taarifa za kiintelejensia kuwa iwapo mikutano hiyo ingeruhusiwa kungekuwa na uvunjifu wa amani.

Hata hivyo, upeo wa kisiasa umebadilika baada ya Rais Samia kuanza kuonyesha mwanga wa maridhiano na kuwapo kwa siasa za kistaarabu, hivyo IGP Wambura moja ya majukumu yake ndani ya Jeshi la Polisi ni kubadilisha mtazamo wa kukabiliana na wanasiasa.

### ULINZI SHIRIKISHI

Jambo lingine ambalo IGP Wambura anapaswa kulitilia mkazo mkubwa ni polisi jamii kwa sababu askari waliopo ni wachache ikilinganishwa na idadi ya wananchi wanaowalinda.

### UCHELEWESHAJI WA KESI

Mtihani mwingine ni kuimarisha kitengo cha upelelezi kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya kesi kucheleweshwa.

### UHALIFU MTANDAONI

Kwa sasa kuna maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia na uhalifu wa mtandaoni unazidi kuongezeka, hivyo lazima jeshi la polisi kujipanga kukabiliana na uhalifu wa aina hiyo.

Haya ndiyo mambo 11 ambayo Wambura akilala akiamka, akiwa ndani ya wadhifa wake mpya, anapaswa kujua kwamba ni baadhi ya vigingi vinavyomkabili katika utekelezaji wa majukumu yake.

### WAMBURA NI NANI?

Wambura ambaye alijiunga na Jeshi la Polisi akiwa kijana baada ya kumaliza masomo yake ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Milambo mkoani Tabora mwishoni mwa miaka ya 1980, kabla ya wadhifa mpya ameshika nyadhifa mbalimbali.

Miongoni mwa nafasi alizoshika hasa baada ya kuhitimu Shahada ya Kwanza ya Sheria (LLB) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni mwendesha mashtaka, Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (OC-CID) Wilaya ya Kipolisi Buguruni, Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai wa Mkoa (RCO) Kinondoni na Manyara na Kamanda wa Polisi Mkoa (RPC) Kinondoni na Arusha.

Zingine ni Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Kanda (ZCO) Maalum ya Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) Makao Makuu ya Polisi.

**TANGAZO**

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 30.06.2022

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 30-Jun-22 | Robo Mwaka ya 31-Mar-22 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,416 | 3,786 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,455 | 7,935 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 38,063 | 32,312 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 7,962 | 3,565 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 12,145 | 9,056 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 73,915 | 70,994 |
| 12 | Mali Nyingine | 30,379 | 42,690 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,483 | 2,611 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **177,817** | **172,949** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 34,756 | 16,000 |
| 18 | Amana za Wateja | 103,858 | 116,726 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 4,121 | 5,628 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 20 | 32 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,401 | 1,796 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 4,012 | 5,315 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,029 | 2,268 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **152,197** | **147,764** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **25,620** | **25,184** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (36,526) | (36,039) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,622 | 699 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,620** | **25,184** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 960,602 | 987,320 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,102 | 4,840 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 493 | 414 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14% | 15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.22% | 6.78% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 0% | 0% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 42% | 41% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70% | 65% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -12% | 2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3% | -3% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-22 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,592 | 3,568 | 7,160 | 5,912 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,157) | (1,063) | (2,220) | (1,805) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,435** | **2,505** | **4,940** | **4,107** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **2,806** | **2,518** | **5,324** | **6,732** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 450 | 414 | 864 | 569 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 2,350 | 2,080 | 4,430 | 6,073 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 6 | 24 | 30 | 90 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(4,205)** | **(4,288)** | **(8,492)** | **(7,148)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,792) | (1,969) | (3,761) | (3,231) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (383) | (393) | (775) | (718) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (2,030) | (1,926) | (3,956) | (3,199) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,036** | **736** | **1,772** | **3,692** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (113) | (37) | (150) | (55) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **923** | **699** | **1,622** | **3,636** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **923** | **699** | **1,622** | **3,636** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 127 | 127 | 127 | 121 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 147 | 111 | 258 | 579 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 7 | 7 | 7 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.53% | 0.40% | 0.92% | 2.20% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3.63% | 2.78% | 6.38% | 13.90% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 65.73% | 70.44% | 68.03% | 56.53% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.06% | 2.23% | 4.18% | 2.98% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo ya Mwaka linganishi 31-Mar-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **923** | **699** | **1,622** | **3,636** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 384 | 173 | 557 | 276 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,921 | (714) | 2,207 | (3,599) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,382 | (6,820) | (2,438) | 19,825 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 5,751 | 3,641 | 9,392 | 1,896 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,761 | (1,029) | 732 | 1,086 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (12,311) | 23,791 | 11,480 | (2,657) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | (37) | (37) | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **3,811** | **19,704** | **23,515** | **20,464** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,869) | (2,332) | (4,201) | (661) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(1,869)** | **(2,332)** | **(4,201)** | **(661)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **1,942** | **17,372** | **19,314** | **18,076** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 47,685 | 30,312 | 30,312 | 86,138 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **49,627** | **47,685** | **49,627** | **104,214** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (36,039) | - | (487) | - | 23,998 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,622 | - | - | - | 1,622 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(34,417)** | **-** | **(487)** | **-** | **25,620** |
| **Mwaka uliopita 2021** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,053) | - | - | - | 23,471 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 1,015 | - | - | - | 1,015 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | 487 | - | - | 487 |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | (487) | - | (487) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(36,039)** | **487** | **(487)** | **-** | **24,485** |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | Imesainiwa | 20Th July 2022 |
| 2 | Fina Andrew<br>**Afisa wa Fedha** | Imesainiwa | 20Th July 2022 |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | Imesainiwa | 20Th July 2022 |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 20Th July 2022 |
| 2 | Oliver Alawuba<br>**Mkurugenzi** | Imesainiwa | 20Th July 2022 |





United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA and Europe.

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana,
- Benin
- Burkina Faso,
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

216952402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu kusikiliza kero za wastaafu umekaa vyema

**SERIKALI** imeanza utaratibu wa kusikiliza kero za wastaafu na kuzishughulikia.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amejipanga kupiga kambi kwenye mikoa mitatu nchini.

Ameanza na kambi hiyo mkoani Dodoma huku miongoni mwa kero zilizoibuka ni kupunjwa mafao.

Katika usikilizaji wa kero hizo kikao kilijumuisha Wakurugenzi na Watendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF.

Hatua hiyo ya Prof. Ndalichako inatokana na kupokea kero mbalimbali za wastaafu, tangu ashike wadhifa katika wizara yake kwa kipindi cha miezi sita.

Hii ni hatua nzuri ambayo inaleta matumaini kwa wananchi kuiamini serikali yao na watendaji wake wanaosikiliza kero zao.

Mtu anapostaafu anategemea mafao yake ndiyo yamwezeshe kuendesha maisha yake mpaka kifo kitakapomfika.

Michango yake anayowekeza katika mifuko ya hifadhi ya jamii anajua ipo salama na hata anapofikia wakati wa kustaafu anajua kuwa fedha zake za mafao atazipata bila usumbufu.

Inapotokea kuwapo usumbufu wa aina yoyote ilhali mstaafu akiwa na taarifa zake zote za kumpatia mafao yake, haipendezi na inavunja moyo kwa wengine wanaowekeza katika mifuko hiyo.

Baadhi ya wastaafu wanalalamika kutopata mafao yao kwa muda wa miaka miwili wakati kimsingi yanatakiwa kulipwa ndani ya siku 60 tangu mtu astaafu.

Hata hivyo, kuna hoja ya vitu vinavyohitajika katika usimamizi wa mifuko ambayo imetakiwa kuwa na kauli moja wakati wanapohudumia wateja wao.

Mfano hoja ya mtumishi aliyekuwa anafanya sekta binafsi, lakini baadaye akaajiriwa serikalini akiwa na umri wa miaka 58, kiutaratibu hulipwa mafao mpaka afikishe miaka 60.

Aidha, mkanganyiko unapotokea, mtu huyo anatakiwa kupata ushauri kwa wataalamu kuhusu mafao yake. Hivyo tunamshukuru Waziri Ndalichako kwa kutoa agizo la kushughulikiwa mafao ya aina hiyo ili yakokotolewe upya.

Waziri Ndalichako, anatarajia pia kuwasikiliza wastaafu kwenye mikoa mingine ya Dar es Salaam na Mwanza ambako kuna wastaafu wengi.

Ameahidi kuangalia changamoto za wastaafu bila kujali walistaafu lini na yeyote mwenye changamoto ya mfuko wa NSSF au PSSSF, serikali itahakikisha inawapatia ufumbuzi ndani ya muda mfupi.


Katika kero hizo Waziri Ndalichako amebaini baadhi ya watumishi walipandishwa vyeo, lakini mshahara haukubadilishwa hadi anastaafu.

Tunapongeza kwa ufafanuzi kuwa mtu wa aina hiyo kama alikuwa mtumishi wa umma na kama alibadilishwa atalipwa malimbikizo yake tangu alipopandishwa cheo hadi anastaafu, pia atalipwa tofauti na makato yake ya awali yaliyotakiwa kulipwa kwenye mifuko na atapa nyongeza katika mafao yake.

Ni matumaini yetu kuwa utaratibu huu utaondoa manung'uniko na vilio kwa wastaafu kucheleweshea mafao yao na baadhi ya kupunjwa.

Ni vyema pia wastaafu wakahakikisha wanahakiki taarifa zao vizuri hata wanapofikia umri wa kupata mafao yao kusitokee tena ucheleweshaji na visingizio visivyokuwa na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusijisahau sana, usafi wa mazingira bado muhimu kutunusuru na maradhi

**KUZINGATIA** suala la usafi wa mazingira ni moja ya namna kuiwezesha jamii kuepuka kupata magonjwa kama ya malaria na yale ya milipuko, vilevile kunusurika na magonjwa hayo, jamii inatakiwa kuweka mazingira katika hali bora, kwenye maeneo yanayowazunguka.

Vilevile, ndani ya mtazano huo wa kuhakikisha jamii haikumbwi na magonjwa, viongozi wa serikali za mitaa nchini, nao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kufanya usafi wa mazingira ndani ya maeneo yao.

Hiyo ni hatua inayoendana na kudhibiti mambo kama kufukia madimbwi ya maji, pia kuteketeza mazalia ya mbu yanayochangia kuongezeka mbu na ugonjwa wa malaria nchini.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema jijini Tanga, alipozindua unyunyizaji wa viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ya mbu kwa wilaya za Tanga, Handeni na Lushoto, iliyofadhiliwa na serikali ya Uswisi, kupitia Shirika la Maendeleo la Uswisi.

Anasema licha ya kutekeleza unyunyiziaji huo wa viuadudu vya kibailojia kwenye mazalia ya mbu, bado jamii inahitajika kuboresha usafi wa mazingira, kwa kuangamiza mazalia ya mbu katika maeneo tunayoishi, hivyo viongozi wa serikali za mitaa wanawajibika kuhimiza usafi wa mazingira.

"Tukifunika madimbwi, itasaidia kuzuia magonjwa yaenezwayo na mbu, pamoja na magonjwa mengine kama dengue, matende na mabusha, homa ya bonde la ufa na chikungunya," anasema.

Hata hivyo, Waziri Ummy anataka kutekelezwe usimamizi wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Anasema, hatua hiyo ikifanyika kikamilifu, itasaidia kupunguza idadi ya mazalia, pia hata wingi wa mbu katika maeneo tunayoishi na hatimaye kupunguza maambukizi ya malaria na magonjwa mengine.

**"Yeyote ambaye hatotekeleza wajibu wake katika kuharibu mazalia ya mbu achukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria hizi," anasema waziri.**

"Yeyote ambaye hatotekeleza wajibu wake katika kuharibu mazalia ya mbu achukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria hizi," anasema waziri.

"Ugonjwa wa malaria bado ni tatizo katika nchi yetu. Hata hivyo, serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria nchini, kati ya watu 100 wanaofika hospitali 10 wana changamoto ya malaria,"anasema.

Ufafanuzi wake unabeba maana kwamba, mradi huo utakuwa wa miaka miwili na utaweza kuleta manufaa yaliyokusudiwa, hivyo kuendelea na afua zingine za udhibiti wa malaria, ikiwemo ya kuwa na mazingira safi.

Lingine kutoka kwa waziri huyo ni kwamba, wizara hiyo kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, unatekeleza mpango mkakati wa malaria wa miaka mitano, unaolenga kupunguza kiwango cha maambukizi ambapo mwaka 2012 kiwango cha malaria kilikuwa asimilia 14 na kupungua hadi kufikia asilimia 7.5 ilipotimu mwaka 2017.

Hapo ndipo Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Didier Chassot, mtazamo wake ni kwamba, wangependa kuiona Tanzania isiyo na malaria na ndio sababu wamefadhili fedha za kitanzania Sh. bilioni 400 kwa ajili ya kutekeleza hatua hiyo kwa kipindi cha miaka miwili, bega kwa bega na serikali nchini.

Hapo akasema, pamoja na juhudi za serikali na washirika wake, kuna ukweli unaobaki kwamba malaria ipo na inasababisha vifo, hata kufika hatua serikali ya Uswisi inaendelea kushirikiana na Tanzania katika harakati za kujikinga na kutokomeza malaria kitaifa.

# Ndalichako aanza kusikiliza kero mafao ya wastaafu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amejipanga kupiga kambi kwenye mikoa mitatu nchini kusikiliza kero za wastaafu na kuzishughulikia.

Prof. Ndalichako alianza kambi hiyo jana mkoani Dodoma huku miongoni mwa kero zilizoibuka kwa wastaafu, ni kudai kupunjwa mafao yao.

Akizungumza katika kikao chake na wastaafu kilichojumuisha Wakurugenzi na Watendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; NSSF na PSSSF, Prof. Ndalichako, alisema kwa kipindi cha miezi sita tangu ateuliwe kushika wadhifa huo, amekuwa akipokea kero mbalimbali za wastaafu.

"Nimeona ni vizuri nitoe nafasi ya kuwasikiliza na kutatua changamoto hizo, nipo na wakurugenzi na wataalamu wangu hapa, changamoto ambazo zipo ndani ya uwezo wangu.

"Kuna wastaafu wanalalamika 'nina mwaka sijapata mafao yangu au nina miaka miwili'. Sasa kama wapo wa namna hiyo, ninaomba walete taarifa zao ili nishughulikie. Kimsingi mafao yanatakiwa kulipwa ndani ya siku 60 tangu mtumishi astaafu," alikumbusha.

Prof. Ndalichako alisema kuna kero zinatatuliwa papo kwa papo na zingine nyaraka zinachukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

"Miongoni mwa wastaafu niliowasilikiza, kuna vitu vinahitajika katika usimamizi wa mifuko tuwe na kauli moja tunapohudumia wateja wetu.

"Kwa mfano, kuna mtumishi alikuwa anafanya sekta binafsi lakini baadaye aliajiriwa serikalini akiwa na umri wa miaka 58, sasa kiutaratibu kulipwa mafao mpaka ufikishe miaka 60 lakini akapata ushauri kwa wataalamu wakamwambia ili kulipwa pensheni yako unapaswa kuendelea kuchangia.

"Amechangia hadi kufika muda wa kustaafu, wakamwambia michango yako hatuitambui na pensheni yako tunakokotoa hadi ulipoishia wakati unahama. Hii ni mikanganyiko ndani ya taasisi.

"Haya ni mapunjo, anapaswa kulipwa hadi alipoongezea, sasa nimeagiza mafao yake yakokotolewe upya hadi michango aliyoelekezwa na taasisi," alisisitiza.

Waziri Ndalichako alisema utaratibu wa kuwasikiliza wastaafu utaendelea kwenye mikoa mingine ya Dar es Salaam na Mwanza ambako kuna wastaafu wengi.

"Tunaangalia kero za wastaafu haijalishi walistaafu lini, yeyote mwenye tatizo na mfuko wa NSSF au PSSSF, tutahakikisha tunawapatia ufumbuzi ndani ya muda mfupi," alisema.

Hata hivyo, alisema katika wastaafu ambao amewasikiliza kwa jana mkoani Dodoma, wengi wana malalamiko ya mapunjo ya mafao na kwamba hali hiyo inatokana na ujumuishaji wa mafao kwenye mifuko waliochangia wastaafu.

"Kuna mapunjo mengine yanatokana na mtumishi aliyepandishwa cheo lakini mshahara wake haukubadilishwa hadi anastaafu, nimepata kesi ya aina hiyo.

"Nimemwambia aende Ofisi ya Rais - Utumishi kwa sababu alikuwa mtumishi wa umma na kama utabadilishwa, atalipwa arrears (malimbikizo) tangu alipopandishwa cheo hadi anastaafu na atalipiwa pia tofauti iliyotakiwa kulipwa kwenye mifuko na sisi tutamwongeza mafao yake," alisema.

Mmoja wa wastaafu, Anamringi Macha, alisema alikuwa mwanachama wa NSSF, alipongeza hatua hiyo ya waziri kusikilizwa kero za wastaafu.

Alisema madai yake ni kupunjwa mafao na ameahidiwa kikokotoo kitafanyika upya kwenye mafao yake.

"Mimi nilikuwa mtumishi wa CCM na ilipofikia Julai mwaka 2018, niliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya nikiwa na miaka 57, lakini nilishawishika kuanza kujichangia mwenyewe kutokana na nafasi niliyoteuliwa haikuwa ya kukata michango na kupeleka kwenye mifuko.

"Nilichangia hadi nilipofika umri wa kustaafu miaka 60, mafao yangu hesabu zake zilipigwa hadi pale nilipokoma utumishi CCM, hii michango ya mbele haikujumuishwa," alisema.

Mstaafu Ramadhan Abdallah ambaye alikuwa mtumishi wa Jeshi la Magereza Msalato, alisema madai yake yalikuwa kupunjwa mafao lakini katika maelezo aliyopewa baada ya kukutana na waziri na wataalamu wa PSSSF, malipo aliyolipwa yako sahihi.


IOGT·NTO·MOVEMENT

## Publication of Bi-Annual Income and Expenditure

**IOGT-NTO Movement** is a Swedish organization, registered in Tanzania as an International NGO, addressing the alcohol harm in Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda, and Uganda. IOGT-NTO Movement works through local partner organizations to fulfil its goal to create strong communities where people are empowered, rights are protected and harm from alcohol and other drugs is minimized. IOGT-NTO has been working in Tanzania since 1993.

**Our Vision:** A democratic world characterized by solidarity and equality where alcohol and other drugs do not impede peoples' welfare, freedom and security.

**Our Mission:** To strengthen relevant actors in their work for reduced use of alcohol and other drugs in developing countries and thus contribute to democratic development, strengthen rights and reduced poverty.

| Bi- Annual Income and Expenditure for the Period for the period from January to June 2022. | |
|---|---|
| **Income:** | |
| Receipt from Donors | 326,409,585 |
| **Expenditure:** | |
| Human Resource | 189,037,230 |
| Office Administration | 78,839,616 |
| Development of IEC materials and Communication | 11,345,860 |
| Monitoring & Follow up on Project implementation and Exit Meetings | 7,819,478 |
| Planning Meetings | 643,000 |
| Partnership and Networking | 7,777,081 |
| Studies and Evaluations | 20,205,627 |
| **Total Expenditure** | **315,667,892** |

**IOGT NTO Movement - East Africa Office**
**Plot No. 204 Lukuledi Road, Regent Estate**
**Box 7522, Dar Es Salaam Tanzania**
**inforoea@iogt.se**
**www.iogtntororelsen.se/**

116953901





Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakipata maelezo mbalimbali kwenye banda la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, katika maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Magari yaliyotumika kukaguliwa Japan kabla kuingia Tanzania

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema kuanzia Julai 20, mwaka huu magari yote yaliyotumika yanayotoka nchini Japani yatakuwa yanakaguliwa nchini humo kabla ya kuja Tanzania kwa utaratibu wa uthibitishaji wa kabla ya usafirishaji ili kuzingatia viwango (PvoC).

Awali utaratibu huo ulikuwa ukitumika nchini, lakini ulibadilika kwa magari yote yanayoingia Tanzania kufanyiwa ukaguzi nchini kwa gharama kati ya Sh. 300,000 hadi Sh. 350,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Meneja wa Usimamizi wa Shehena zinazoingia na kutoka nchini, Mhandisi Saidi Mkwawa, alisema ukaguzi wa magari hayo utafanywa na kampuni ya nchini Japan ya EAA Company Limited kuanzia tarehe tajwa.

"Magari ambayo tayari yalikuwa yameshanunuliwa na yako kwenye mchakato wa kusafirishwa au yalishapakiwa kwenye meli kwa ajili ya kusafirishwa kuja hapa nchini kabla ya Julai 20, mwaka huu, yatakapofika yatakaguliwa na TBS bila adhabu yoyote," alisema Mkwawa.

Aliongeza kuwa utaratibu huo wa kukagua magari kabla hayajawasili nchini utasaidia kuepuka gharama za matengenezo kwa wanunuaji wa magari.

Aidha, alibainisha kuwa shirika hilo linaendelea na taratibu za kupata mawakala kwa ajili ya ukaguzi wa magari yanayotoka nchi za Uingereza, Dubai na Singapore na kwamba utaratibu wa nchi hizo utakapokamilika waingizaji na wafanyabiashara wa bidhaa hiyo watataarifiwa.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

DOCG

**TANGAZO LA KAZI KWA AFISA UHUSIANO WA JAMII**
**REJEA NO. MST-TZ-202 20 720**

Kampuni ya Daqing Oilfield Construction Group Co., Ltd. (hapa kama DOCG), ikiwa ni MKANDARASI wa Hifadhi ya Kituo cha Mradi wa EACOP, inawakaribisha wagombea wenye uzoefu na sifa nzuri kuomba nafasi za **AFISA UHUSIANO WA JAMII (2)** nafasi mbili ambazo zitakuwa mkoani Tanga. katika kata ya Chongoleani . Watanzania wote wenye sifa zifuatazo na ambao wako tayari kufanya kazi kwenye Mradi wa Kituo na Hifadhi (MST) ulioko Chongoleani wanapaswa kutuma maombi.

**1.0 Nafasi - Afisa Uhusiano wa Jamii (Nafasi 2)**

**1.1 Sifa:-**

- Shahada ya kwanza katika Sayansi ya Jamii , Sosholojia, sayansi ya mazingira au taaluma nyingine inayofaa.
- Angalau miaka 5 ya uzoefu wa kitaalamu kuendesha ushiriki wa washikadau katika jumuiya za vijijini.
- Angalau miaka 3 ya uzoefu unaohusiana na ujenzi unayopendelea.
- Uzoefu wa kufanya shughuli za ushirikishwaji na mamlaka ikijumuisha itifaki zinazohusiana .
- Kiwango cha juu cha ustadi baina ya watu na uwezo uliothibitishwa wa kukuza na kudumisha uhusiano mzuri na anuwai na washikadau ikijumuisha busara ya hali ya juu, Diplomasia na uwezo wa Kudhibiti migogoro na kupata maelewano, inahitajika.
- Kiwango cha juu cha ushirika na uwezo wa kupanga kazi ya timu na malengo muhimu.
- Ujuzi bora wa Kiingereza na Kiswahili kilichoandikwa na kuzungumza.

**1.2 Majukumu:-**

- Kukuza uelewa wa wadau wa ngazi ya Wilaya, Kata, Kijiji na Hamlet na jinsi wanavyoweza kuathiriwa na shughuli za DOCG.
- Kuza uelewa wa shughuli za ujenzi wa DOCG, maeneo yote ya kazi ya DOCG (ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja) na aina ya ushirikishwaji wa jamii unaohitajika, ijulishe jamii kuhusu shughuli za DOCG.
- Tekeleza mpango kazi wa ushirikishaji wa wadau wa DOCG
- Muunganisho na mwakilishi wa Site wa DOCG na afisa uhusiano wa jamii wa EACOP kuhusu shughuli za ujenzi.
- Weka DOCG ikisasishwa kuhusu masuala ya jumuiya na kuangazia hatari inayoweza kuhusishwa na jumuiya kwa DOCG kwa hatua.
- Rekodi na uripoti maswali ya jumuiya na masuala yanayohusiana na mradi na ushiriki katika kuandaa na kutoa majibu kwa wakati.
- Tekeleza Utaratibu wa Malalamiko wa Mradi wa EACOP.
- Kuratibu na EACOP katika kutatua kero inayohusiana na shughuli za DOCG.
- Dumisha rekodi za kina taarifa zote za ushiriki wa washikadau ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za mikutano, Rejesta za Mahudhurio, Picha na rekodi zilizoandikwa na kutunza hifadhidata kwa bidii/nakala laini kwa kushiriki na EACOP.
- Kutunza rejista ya na kurekodi maswala yote ya washikadau, masuala na maoni mengine yoyote ya washikadau yanayohusiana na shughuli za ujenzi wa DOCG ili kuchukuliwa hatua na Meneja wa Kijamii wa DOCG.
- Toa ushiriki wa kila siku, kila wiki na kila mwezi wa wadau wa ujenzi katika kuweka ripoti inavyohitajika.
- Saidia shughuli za ujenzi wa DOCG na shughuli za ushiriki kama inavyohitajika na Meneja wa Kijamii wa DOCG na Meneja wa Ujenzi wa DOCG.

**1.3 Muda**
Mkataba utakuwa wa kazi maalum (Kipindi cha Ujenzi)

**1.4 Aina ya kazi**
Ajira ya wakati wote

**1.5 Mzunguko wa Kazi**
Atakuwa akifanya kazi siku 26 ( ishirini na sita ) mfululizo na siku 4 (nne) za mapumziko

**1.6 Mahali pa Kazi**
Chongoleani mkoani Tanga.

Watu wanaovutiwa na wenye uwezo na nia ya kufanya kazi na DOCG katika nafasi iliyotajwa hapo juu kwenye kituo cha kuhifadhia maji ya Baharini (MST) wanapaswa kukomesha maombi na CV kwa Ofisi ya Rasilimali Watu ya DOCG kupitia barua pepe. **frank.david@docgi.cn** saa au kabla ya saa 17:00 kwa Saa za Afrika Mashariki (EAT), kuwasha **Tarehe 3 Agosti 2022** . _ Mada ya barua pepe inapaswa kuwa **MST-TZ-20220 720_ Kazi Ombi la CLO_ NAME .**

**WANAWAKE WANAHIMIZWA KUOMBA MAOMBI.**

**Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi itakuwa siku 14 kutoka siku ya tangazo.**
**TAARIFA; HAKUNA KUAJIRI MLANGON.**
**Maombi ni bure kabisa, usilipe kuomba au kupata kazi.**
**Kwa maswali ( saa za kazi): 0692117239, 0652178898 & 0734 130267**

**Imetolewa na; -**
**Afisa Rasilimali Watu (Daqing Oilfield Construction Group Co., L td)**
**Katika siku hii ya 19 ya Julai, 2022.**

216954302

# Watakiwa kuchangamkia soko la SADC

**Na Mary Geofrey**

WAKUU wa mikoa ya Songwe na Mbeya wamewataka wakulima na wawekezaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kuzalishaji mazao yenye tija ili yaingizwe katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza mkutano wa siku mbili wa wadau wa sekta hizo ulioandaliwa na Kituo ya Kuendeleza Kilimo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (SAGCOT), walisema wadau wa sekta hizo wanapaswa kutumia fursa ya soko la SADC kuuza mazao na kuiletea nchi faida.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Rukwa, iko katika lango la kuingilia soko la SADC.

"Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini una jiografia nzuri katika uzalishaji wa mazao ya chakula, matunda na mboga, hivyo wakulima watumie fursa hii kuzalisha mazao kwa tija na kuingiza kwenye soko la ushindani jambo litakaloongeza kwa kipato cha mkulima na kupunguza wimbi la umaskini nchini," alisema Homera.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema mikutano ya namna hii ni muhimu kufanyika mara kwa mara kwa sababu inasaidia kuibua changamoto na kukubaliana namna bora ya kufikia malengo kwa pamoja.

"Tulikubaliana kuwa na mazao ya mkakati katika mikoa ya Mbeya na Songwe, kwa kushirikiana na SAGCOT na wadau wengine wa sekta za kilimo mifugo na uvuvi hivyo kuna kila sababu ya kuendeleza majadiliano ili mkakati uliopo kwenye mazao uweze kutekelezeka," alisema Mgumba.

Aliyataja mazao hayo ni pamoja na parachichi, alizeti, mpunga, maziwa, kuku na viazi mviringo na kwamba lengo la mkataba ulioingiwa mwaka 2020 ulilenga kutatua changamoto ilikuwapo ya upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa mkulima ya mazao hayo pamoja na uzalisha wenye tija sokoni.

Naye Mkuu wa Kongani na Ubia wa SAGCOT, Maria Ijumba, alisema mkataba walisainiana kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, wakulima na watoa huduma imezaa matunda kwa sababu mazao ya mkakati katika ukanda huo yameweza kupata soko ndani na nje nchi.

Naye Meneja wa Kongani ya Mbarali, Tullah Mloge, alisema katika mkataba huo SAGCOT imeshirikiana pia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), Kituo cha Uwekezaji (TIC) katika kuhakikisha tunapata masoko ya uhakika ya mazao na bidhaa za wakulima.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi Bajaji kwa Omar Idi, iliyotolewa na Benki ya NMB Mpango Maalum kwa vijana wa Go na NMB, alipotembelea miradi ya maendeleo inayoendelea Unguja na Pemba juzi. Kushoto ni Meneja wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Shame. Benki hiyo, pia imekabidhi pikipiki 5 na bajaji moja kwa wajasiriamali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mawaziri EAC wakutana maazimio mkutano wa 22

**Na Mwandishi Maalum,** ARUSHA

KUELEKEA Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kinachofanyika leo na kesho jijini Arusha, mawaziri wa jumuiya hiyo wamekutana kukamilisha baadhi ya maazimio yanayotarajiwa kuwasilishwa kwa wakuu hao wa nchi wanachama.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Balozi Liberata Mulamula, alisema jana kuwa kikao cha mawaziri wa jumuiya hiyo ni shirikishi kati ya serikali, sekta binafsi na wadau wengine vikiwamo vyombo vya habari.

Wahariri wa vyombo vya habari ni miongoni mwa wadau walioalikwa kushiriki mkutano huo wa mawaziri kwa lengo la kupata mawazo kuhusu namna bora ya kuvishirikisha vyombo vya habari katika shughuli za jumuiya ili kuwawezesha wananchi kutoka nchi wanachama kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu fursa zilizopo katika jumuiya hiyo.

Wakuu hao wa nchi pia wanatarajiwa kuzindua barabara ya mzunguko ya Arusha ambapo Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, alisema jana kuwa hiyo ni fursa muhimu kwa ukuaji wa biashara katika jumuiya hiyo.

Katika mkutano huo wa 22 wa kawaida, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwa mara ya kwanza itahudhuria kama mwanachama mpya wa jumuiya hiyo ambayo kwa sasa inaundwa na nchi saba.

# Watanzania waonyeshwa fursa masomo Georgia na India

**Na Joseph Mwendapole**

VIJANA wa Tanzania wanaomaliza elimu ya sekondari wameshauriwa kuchangamkia fursa mbalimbali za masomo ya elimu ya juu yanayotolewa kwa gharama nafuu nchini Georgia na India.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, wakati akizungumza kwenye maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam.

Mollel alisema nchi za Ulaya kama Georgia ni tajiri lakini ina changamoto ya kupata nguvu kazi na ili nchi iendelee kupiga hatua, hivyo inahitaji nguvu kazi kubwa zaidi.

Alisema nchi hiyo pamoja na utajiri ina watu milioni nne, inahitaji nguvu kazi kubwa, hivyo Watanzania watakaopata fursa ya kusoma nchini humo watakuwa na nafasi kupata kazi moja kwa moja.

Kwa mujibu wa Mollel, faida nyingine ya kwenda kusoma nchini Georgia ni kwamba mtu akipata kibali cha ukaazi, ni rahisi kupata VISA ya Shengen ambayo inamwezesha mhusika kuzunguka zaidi ya nchi 30 mwanachama wa Shengen zikiwamo Ufaransa, Ujerumani, Hungary Italia na Polland.

Alisema hizo ni nchi tajiri na zenye teknolojia ya hali ya juu lakini nazo zinakabiliwa na uhaba wa nguvu kazi hivyo kwa kijana kwenda kusoma nchini Georgia anakuwa amejiweka kwenye mazingira mazuri ya kupata utaalamu na ajira pia.

"Sasa maana yake wanatuhitaji hivyo tukisoma karibu yao tukajua mila na tamaduni zao maana yake tutajifunza pia fursa zao na tukijifunza fursa zao na kuchukua wawekezaji kutoka kwao na kuja kuwekeza kwetu," alisema na kuongeza.

"Kwenda nje kusoma si kwenda na kurudi na cheti tu hapana. Sisi Global tunataka mwanafunzi akienda kusoma nje ya nchi arudi na mwekezaji, arudi na fursa ya kuwekeza kusaidia vijana wenzake na wawe mawakala wa bidhaa za viwandani za huko walikosoma," alisema Mollel.

"Kwa hiyo nje ya nchi siyo elimu tu yenye neno cheti ni elimu kwenye nchi tajiri zenye teknolojia ya hali ya juu na kuzibeba fursa na kuzileta kwetu kwa sababu nchi yetu ina sera nzuri na viongozi mahiri kilichobaki ni sisi kwenda kuchukua fursa hizo,"alisema.

**KUHUSU VYUO VYA INDIA**

Mollel alisema India kuna zaidi ya vyuo vya elimu ya juu zaidi ya 80,000 na vyuo vikuu 4,000 na GEL imefanikiwa kuleta kwenye maonyesho hayo vyuo bora zaidi kutoka nchini humo vilivyobobea kwenye nishati.

"Tunapozungumzia vyuo vikuu bora hatuzungumzii vile vinavyotoa kozi za aina moja, ndani ya maonyesho haya GEL tuna vyuo vikuu vilivyobobea kwenye mafuta na gesi na nishati tu hivyo wanafunzi wanaohitaji kusoma kozi za nishati, kwa upande wa sola, nishati kwenye upepo au kwenye maji chuo kilichobobea ambacho hata wao wanakitegemea kuleta mabadiliko kwenye nishati katika nchi yao kipo hapa kwenye maonyesho," alisema.

Mollel alisema chuo kilichobobea kwenye uhandisi wa meli kutoka India nacho kiko kwenye maonyesho hayo kwaajili ya kunyesha kwa Watanzania fursa zilizoko na namna wanavyoweza kujiunga nacho kwa masomo ya uhandisi.

Alisema pia kuna Chuo Kikuu bora cha Teknolojia cha Lovely Professional University chenye wanafunzi 40,000 ndani ya kampasi moja na kimehudhuria ndani ya maonyesho ya vyuo vikuu mwaka huu.

"Ukitafuta vyuo vikuu vya namna hii duniani unaweza kukuta havifiki hata 60 dunia nzima chuo kikuu ndani ya kampasi moja wanafunzi zaidi ya 40,000 siyo kawaida, hivi vyuo vikuu ada ni dola 2,000 tu na hosteli unaweza kukuta ni 3,000,000 mwanafuinzi anauwezo wa kusoma kozi aina yoyote," alisema Mollel.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza kwenye sekta ya afya kwa kiwango kikubwa na sasa kila kanda inahospitali kubwa na nzuri zenye vifaa vya kila aina na hospitali za rufani za kutosha.

"Tanzania tunahitaji kuwekeza kwenye Medical Tourism na nchi tunahitaji watu kuoka Rwanda, Burundi, Malawi, Kenya na chi jirani yetu zitegemee matibabu kutoka kwenye nchi yetu lakini kuna baadhi ya kozi za afya ambazo India inachukua kama fursa kwa kupeleka watu wakasome kule," alisema.

"Leo ninavyoongea chuo kikuu kikubwa kinachotoa kozi za afya ambazo kwa vyuo vikuu vya Tanzania bado havijaanza kuzitoa vipo kwenye maonyesho haya ndani ya mabanda ya GEL na uwepo wa vyuo hivi unawasaidia wanafunzi kupata udahili wa papo hapo na kusaidia vyuo vya ndani kushirikiana na vya nje kuchota teknolojia waliyo nayo na kuileta hapa," alisema.

# Serikali kuzalisha mbegu za miwa

Na Mary Geofrey

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali itaanza kuzalisha mbegu za miwa kwa kutumia kitalu wilayani Kilombero mkoani Morogoro.

Bashe alitoa ahadi hiyo juzi wilayani humo wakati wa kikao kazi cha kujadili kero zinazowakabili wakulima wa miwa na kubainisha kuwa wamefikia hatua hiyo baada ya Kampuni ya Sukari Kilombero kutoa ekari 400, ili kuiwezesha serikali kutekeleza mradi huo.

"Ubora wa miwa ni mchakato kuanzia mbegu iliyopandwa, namna ulivyolima, namna ulivyovuna na namna unavyopeleka kiwandani.

"Nimesikia kilio cha upatikanaji wa mbegu, tunaanzisha kitalu cha serikali cha uzalishaji wa mbegu hapa kwenu," alisema.

Waziri Bashe alisema hatua hiyo imefikiwa na serikali baada ya wakulima kuwasilisha kero zao za upatikanaji wa mbegu bora, tatizo linalochangiwa na ukosefu wa mitaji na utaalamu wa kuzalisha mbegu bora, hivyo kuathiri ubora wa mavuno yao.

Kuhusu upatikanaji wa mbolea, Bashe aliahidi kuwa serikali inaendelea na mpango wa kuanzisha ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote nchini ambayo itawanufaisha wakulima hao na kutatua tatizo lililoko la ongezeko la bei.

Bashe pia aliahidi serikali itashirikiana kwa karibu na Kampuni ya Sukari Kilombero katika kutengeneza mfumo utakaohakikisha uwazi kwenye vipimo vya ubora wa miwa ili kuwahakikishia wakulima kuwa wanalipwa kiasi stahiki kulingana na kiwango cha sukari kwenye miwa yao.

"Serikali itaunda kikosi kitakachofanya kazi na KSCL na kuripoti matokeo ya vipimo vya ubora wa miwa kwa wakulima hao wa nje," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhusiano wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Ephraim Mafuru, alisema wanafanya mazungumzo ili kuingia makubaliano ya ununuzi wa pamoja wa pembejeo kati ya kampuni hiyo na wakulima.

Alisema ununuzi wa pamoja utasaidia wakulima kupata pembejeo za kilimo kwa wakati unaostahili.

"Mkataba huu utaainisha muundo wa upatikanaji wa gharama za mtaji na bohari kulingana na miongozo kutoka mamlaka husika," alisema Mafuru.

## TRA yawahamasisha wananchi kudai risiti

Na Elizabeth Zaya

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imeanzisha kampeni maalum ya kuhamasisha wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa au kupatiwa huduma yoyote, ikipewa jina la 'Dai Risiti Halali ya EFD, Ushinde Pesa'.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo iliyoanza rasmi katika Mkoa wa Kikodi wa Tegeta, Mkurugenzi wa Utafiti, Sera na Mipango wa TRA, Ephraim Mdee, alisema juzi kuwa katika kampeni hiyo maalum, watakuwa wanatoa zawadi ya pesa kwa wananchi wanne ambao wataonekana kuwa vinara wa kudai risiti hizo pale wanaponunua bidhaa au kupatiwa huduma yoyote.

Alisema zawadi kwa washindi hao itakuwa ikitolewa kila siku ya Jumatatu kila wiki kwa kuchezesha droo ya moja kwa moja kupitia risiti zao.

"Kwa kuzindua rasmi kampeni hii maalum, tayari tumechezesha droo ya kwanza na kupata washindi wanne ambao kila mmoja amepatiwa Sh. 250,000," alisema Mdee.

Alisema kila wiki watakuwa wanatoa washindi wanne na kwamba kila mwisho wa mwezi watakuwa wanachezesha droo kubwa ya kumpata mshindi mmoja wa Sh. milioni moja.

Alisema kampeni hiyo imeanza mwezi huu na inatarajia kumalizika Septemba mwaka huu, ikianzia Dar es Salaam na baadaye wataipeleka katika mikoa yote nchini.

"Tumeanza kampeni hii Dar es Salaam kama kianzio kwa Mkoa wa Kikodi wa Tegeta lakini tunatarajia kwamba tuipeleke mikoa yote Tanzania kwa sababu lengo lake ni kuhamasisha wananchi kujenga tabia ya kudai risiti. Na tunataka hata wenyewe kwa wenyewe wawe wanahamasishana," alisema Mdee.

Kaimu Meneja wa Mkoa wa Kikodi Tegeta, Mazula Mtwale, alisema katika kampeni hiyo ya kwanza, washindi wanatakiwa kutoka katika maeneo yote yalipo katika mkoa huo.

Alitaja baadhi ya maeneo hayo yaliyopo kwenye mkoa huo wa kikodi ambao wananchi wanapaswa kushiriki kwenye kampeni hiyo ya kianzio kuwa ni Tegeta, Salasala, Kunduchi, Mambwepande, Madale, Wazo, Mbopo, Mbweni, Mbezi Beach, Bahari Beach, Boko na Bunju.




Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Prof. Neema Mori (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela na Meneja Mipango ya Biashara wa benki hiyo, Masele Msita, wakifurahia tuzo ya 'Benki Bora Tanzania' katika hafla ya kuwashukuru wateja na wadau kwa mafanikio hayo, jijini Dar es Salaam jana. Jarida maarafu la fedha na uchumi la Euromoney liliitaja CRDB kama moja ya benki bora duniani wakati wa kukabidhi tuzo kwa benki zilizofanya vizuri Julai 13, 2022, jijini London, nchini Uingereza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yashukuru wateja kwa tuzo

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya CRDB imewashukuru wateja na wadau wake baada ya kutunukiwa tuzo ya 'Benki Bora Tanzania' na jarida maarufu la masuala ya fedha na uchumi la Uingereza la Euromoney.

Shukrani hizo zilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wajumbe wa bodi, wafanyakazi na wateja wa benki hiyo.

Akizungumza katika mkutano huo, Nsekela alisema wateja wa benki hiyo wamekuwa sehemu ya mafanikio ya utekelezaji wa mkakati wa mageuzi ya biashara ambao umewezesha kupata tuzo hiyo.

"Niwashukuru wateja, wanahisa, serikali, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na washirika wetu wa biashara kwa ushirikiano wanaotupa na kuendelea kutufanya kuwa bora zaidi. Hii siyo tuzo ya Benki ya CRDB peke yake, ni tuzo ya Watanzania wote," alisema Nsekela.

Mwaka 2019, benki hiyo ilianza kufanya mageuzi katika biashara yake ambayo yamejikita katika kutengeneza thamani endelevu, kuongeza ujumuishi wa kifedha na kujenga uchumi jumuishi kupitia bidhaa, huduma na mifumo bunifu ya utoaji huduma.

"Tuzo ya Euromoney inathibitisha nafasi ya Benki ya CRDB kama benki kiongozi nchini. Vilevile, inatambua mafanikio ya mageuzi haya ambayo yamepelekea ukuaji endelevu wa benki yetu na ukinufaisha wateja, wawekezaji na uchumi wa nchi kwa ujumla wake," alisema.

Waandaaji wa tuzo hizo pia wametambua mchango wa mageuzi wa kidijitali ambayo yamefanyika ndani ya Benki ya CRDB, ikielezwa kuwa kiasi kikubwa yamesaidia kuchochea ongezeko la ujumuishi wa kifedha nchini.

"Tumekuwa pia tukishiriki kikamilifu katika kusaidia sekta mbalimbali za maendeleo nchini hususani kilimo na ujasiriamali ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa taifa letu," alisema Nsekela huku akibainisha kuwa benki hiyo ilitoa ahueni kubwa kwa sekta ya biashara nchini katika kipindi cha janga la UVIKO-19.

Alisema benki hiyo pia imetambuliwa kwa kuwa na uwezo mkubwa katika uwezeshaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali na sekta binafsi, akitolea mfano mradi wa umeme wa maji wa Bwawa la Nyerere na mradi wa Reli ya Kisasa (SGR).

Nsekela alisema jitihada na mafanikio hayo pia zimekuwa zikijidhihirisha katika matokeo ya kifedha ambayo imekuwa ikiyapata mwaka hadi mwaka.

Benki ya CRDB ni benki ya kwanza nchini kutunikiwa tuzo ya Benki Bora Tanzania na Euromoney mwaka 2004. Nsekela alisema ushindi wa tuzo hiyo mwaka huu unadhihirisha kuimarika kwa utendaji wa benki siku za hivi karibuni na kutambuliwa kimataifa.

Mwaka jana, benki hiyo ilitajwa kama Benki Bora Tanzania na benki inayoongoza kwa ubunifu na jarida maarufu duniani la masuala ya fedha la Global Finance, huku Taasisi ya Utafiti wa Ubora barani Ulaya ikiitunuku benki hiyo Tuzo ya Ubora.

# Mpango atoa tahadhari uchafuzi plastiki baharini

**Na Joseph Mwendapole**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema dunia inapaswa kuunganisha nguvu kulinda mazingira ya bahari dhidi ya uchafuzi wowote, vinginevyo ifikapo mwaka 2050, bahari itakuwa imejaa taka za plastiki.

Alitoa angalizo hilo jana wakati akifungua kongamano la kimataifa la siku 10 kuhusu namna sahihi ya kulinda mazingira ya bahari dhidi ya uchafuzi unaotokana na shughuli za binadamu kama uvuvi, usafiri na utalii.

Kongamano hilo linawashirikisha wataalamu mbalimbali wa masuala ya mazingira kutoka mataifa mbalimbali, likifadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Idara ya Sheria ya Bahari.

Dk. Mpango alisema kuna umuhimu wa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha inazingatia matumizi sahihi ya bahari ambayo ni muhimu kwa chakula, usafiri na rasilimali nyinginezo ili iwe endelevu kwa vizazi vijavyo.

"Binafsi ninaona mkutano huu umekuja wakati mwafaka na ninawapongeza Umoja wa Mataifa kwa kufadhili mkutano huu na kuamua kuufanyia hapa Tanzania. Sisi sote ni wanufaika wa kuwapo kwa bahari na ikiharibika wote tutakuwa waathirika," alitoa angalizo.

Dk. Mpango alisema Serikali ya Tanzania imejitahidi kupiga vita matumizi ya mifuko ya plastiki kama sehemu ya mkakati wa kulinda mazingira ya bahari na mazingira kwa ujumla ili yanufaishe vizazi vijavyo.

Alisema serikali imepiga marufuku uvuvi haramu ukiwamo wa kutumia baruti na imekuwa ikifanya doria za mara kwa mara kuhakikisha hakuna uvunjaji wa sheria.

"Taifa moja pekee haliwezi kupambana na kufanikiwa kulinda bahari, hili linahitaji jitihada za pamoja kwa mataifa yote kwa sababu kila mmoja ni mnufaika wa bahari. Tunatakiwa kujengeana uwezo wa kukabiliana na vitendo vya uchafuzi wa bahari.

"Lazima dunia iweke mipango itakayohakikisha shughuli za kiuchumi baharini kama uvuvi unaendelea kama kawaida na bahari inakuwa salama na lazima tutambue kwamba wakati wa kuchukua hatua kulinda bahari ni sasa," alihimiza.

Alisema baadhi ya nchi zinashindwa kukabiliana na uchafuzi wa bahari kutokana na vikwazo vya kiuchumi, teknolojia na menejimenti, hivyo nchi zenye uwezo zinapaswa kusaidia kuzijengea uwezo wa kiteknolojia na kifedha mataifa hayo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Dk. Selemani Jafo, alisema serikali inajitahidi kujenga miundombinu yake kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na bwawa la kuzalisha umeme wa Megawati 2,115 huko Rufiji mkoani Pwani.

Alipongeza hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kushirikiana na jumuiya ya kimataifa na kushiriki mikutano mbalimbali yenye ajenda ya kulinda mazingira na kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya gesi kama njia ya kulinda mazingira.

Alisema serikali pia imeweka kipaumbele kwenye sekta ya kilimo na kwamba ushahidi wa hilo ni namna ambavyo imekuwa ikiongeza bajeti ya kilimo mwaka hadi mwaka.




Mkurugenzi wa Idara ya Uhusiano wa kampuni ya Sukari ya Kilombero, Ephraim Mafuru (katikati), akijadiliana jambo na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), katika mkutano na wakulima wa miwa wa Kilombero, mkoani Morogoro mapema wiki hii. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manispaa ya Morogoro kukusanya bilioni 86/-

**Na Christina Haule,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro inatarajia kukusanya Sh. bilioni 86.76 katika mwaka wa fedha 2022/23 ili kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, alibainisha hayo jana kwenye mkutano wa kawaida wa mwaka wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Alifafanua kuwa kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 12.654 zitatokana na mapato ya ndani, mishahara ni Sh. bilioni 64.423, matumizi mengineyo Sh. bilioni 1.164 na miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 8.519.

Kihanga alisema manispaa hiyo imeweka vipaumbele katika maeneo sita ambayo ni makusanyo ya mapato, elimu, afya, usafi wa mji na utunzaji wa mazingira, utawala bora na mipango miji.

Alisema kupitia fedha hizo, pia watamalizia miradi isiyokamilika ikiwamo ujenzi wa Kituo cha Afya Tungi, Kumaliza miundombinu ya Zahanati ya Mji Mkuu, Kauzeni, Mafiga na Kihonda sambamba na kumalizia ujenzi wa maboma hamsini ya madarasa ya shule za msingi.

Kihanga alisema katika utekelezaji wake, halmashauri kupitia wataalamu wake wa ndani katika mwaka wa fedha 2021/22, imepanga na kupima viwanja 12,000 katika shamba la Tungi Sisal Estate kwenye eneo la ukubwa wa ekari 4,500 katika Kata ya Kihonda, Mtaa wa Kiegea A na Kata Mkundi, Mtaa wa Kiegea B.

Alisema kwa kushirikiana na sekta binafsi, zaidi ya vipande 36,310 vya ardhi vimetambuliwa katika mitaa mbalimbali ndani ya manispaa hiyo katika maeneo yaliyojengwa kiholela.

Alibainisha kuwa mwaka wa fedha 2021/22, halmashauri ilifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya Sh. bilioni 65.971 sawa na asilimia 83.4 ya makadirio ya makusanyo ya Sh. bilioni 74.629.

Kihanga alisema fedha hizo zilitumika katika mishahara, matumizi ya ruzuku, matumizi yasiyo na ruzuku pamoja na miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Juni 2022, halmashauri ilikuwa imetumia Sh. bilioni 59.675, sawa na asilimia 83.83.

Alisema Manispaa ya Morogoro kupitia fedha za miradi kutoka Serikali Kuu, ilipokea Sh. milioni 940 zikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa shule mpya mbili za Mindu na Lukobe.

Alisema fedha hizo zitaboresha miundombinu ya elimu ya sekondari ndani ya manispaa ambapo ujenzi wa vyumba 16 vya madarasa, maabara sita, maktaba mbili, vyumba viwili vya Tehama, majengo mawili ya utawala na matundu 40 ya vyoo unaendeleo vizuri ukiwa kwenye hatua ya upauaji.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Morogoro, Sylvester Yaredi, aliwataka madiwani kufanya kazi kwa ushirikiano ili kutimiza malengo na ilani ya chama kama inavyokusudiwa ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Diwani wa Sabasaba, Yahaya Lukwele, alichaguliwa kwa kura zote za ndiyo na madiwani 38 kuendelea kuwa Naibu Meya wa Halmashauri hiyo katika kipindi cha mwaka 2022/23 kutokana na ushirikiano aliounyesha katika utendaji kazi kwenye nafasi yake.

# Taasisi yawawezesha wanawake kiuchumi na kuwania uongozi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Star Woman Foundation imetoa mafunzo ya uongozi na uchumi kwa wanawake ili kutoziogopa nafasi za uongozi katika jamii zinapotangazwa.

Mratibu wa mafunzo wa taasisi hiyo, Anne Mamkwe, akizungumza jana na wanawake zaidi ya 50 kutoka Wilaya ya Iringa, alisema mbali ya hamasa kubwa iliyoko kutokana na uongozi mzuri wa wanawake chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, mwitikio sio mkubwa wa wanawake kugombea.

Alisema kupitia mafunzo yanayotolewa na taasisi yake yatasaidia wanawake zaidi kutobaki nyuma nafasi za uongozi zinapotangazwa.

Mamkwe alisema kwa Tanzania wanawake wanajivunia uongozi wa Rais Samia na baadhi ya mawaziri, wakuu wa wilaya na mikoa ambao wanafanya vizuri kwenye nafasi zao wanazoongoza.

Kupitia mfano mzuri wa viongozi hao na mafunzo mbalimbali yanayotolewa na taasisi yake, wanaamini mwitikio kwenye chaguzi mbalimbali mwamko wa wanawake utakuwa mkubwa zaidi.

Alisema taasisi yake inaamini katika kumwelimisha mwanamke kama sehemu ya ukombozi wa kweli kwenye familia na jamii.

Alifafanua kuwa sehemu kubwa ya wanawake ndiyo nguzo ya familia mwanamke akiwa mbele kuongoza ni ukweli usiopingika kuwa maendeleo yatazidi kuchipua. "Tunaendelea kutoa mafunzo haya ya uongozi na uchumi kwa wanawake na tumekwisha toa mafunzo kama haya kwenye mikoa mbalimbali ya Tanzania ukiwamo Mkoa wa Dar es Salaam na sasa Iringa."

Awali, akitoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwenye mafunzo hayo, Christina Onyango, kutoka dawati la jinsia, Mkoa wa Dar es Salaam, alisema wanawake wana wajibu mkubwa wa kutokomeza ukatili kwa kuwaibua wanaume wanaofanya ukatili kwenye familia.

Alisema suala la ukatili wa kijinsia limekuwa likifanyika kwenye jamii na baadhi ya wanawake hutetea wanaotekeleza ukatili huo.

Kwa upande wao Neema Kibasa na Mariam Mhagama, wakizungumza kwa niaba ya washiriki wenzao, walisema kupitia elimu waliyoipata wanaamini watakwenda kufikisha kwa wenzao na kuona wanajiamini na kujitambua zaidi.



Ukurasa 12

Mradi maji, ulivyo na kasi kukabili mabadiliko ya tabianchi Simiyu




Ukurasa 13

**KILICHOJIRI ZIARA YA MARIA STOPES**

....Mkutano wa kijijini ulivyoanika siri utitiri wa mimba katika wilaya



Ukurasa 14

**MKUTANO WABUNGE VS WANAHARAKATI**

**Uhaba wa matundu vyoo kwa vijana, unavyowaibulia madhila kijinsia shule**

AFYA

# Sakata wanakijiji wafunguka mkutanoni wajawazito zahanati wafungiwa nje usiku

**Na Neema Hussein, Mlele**

• Kuingia?... Mpaka afike na kiongozi • Kisa? Jibu 'ndio, hapana' zapishana



Vijana wakieleza changamoto zao na kupewa elimu ya afya ya uzazi na ukatili wa kijinsia kijijini Mapili, wilaya ya Mlele, Katavi. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

NI taarifa zinazotajwa zenye ukakasi kijamii, kuwapo kasi kubwa ya mimba za utotoni hata kufika hatua kuwainua wadau wa afya ya jamii, Maria Stopes nao 'kiguu na njia' hadi wilayani Mlele mkoa wa Katavi, kujua kilichoko huko na msingi wa shida yao.

Ni safari inayowafikisha hadi kijini Mapili katika kata la Ilela katika Halmashauri ya Wilaya Mlele, kudadisi na kushuhudia kilichoko, wahusika Maria Stopes wakikiri wameshindwa kuvumilia taarifa ya idadi kubwa ya watoto wa kike wanaopewa mimba.

Maofisa wa shirika hilo baada kufika kijijini, wakaomba kukutana na makundi ya watu mahali hapo, lengo kubwa ni kufahamu kwa kina changamoto zao na sababu ya kukithiri mimba za watoto, ili kupata majibu ya matatizo yao, namna ya kuwakomboa kuanzia elimu ya afya ya uzazi, pia ukatili wa kijinsia.

Mchakato ulivyo; Siku ya kwanza Maria Stopes ilikutana na vijana wa kike na kiume; siku ya pili wazazi; siku ya tatu wazee wa kimila, viongozi wa dini na kijiji; na siku ya nne ikawa mahsusi wawakilishi wa makundi, wakuu wa idara serikalini, mashirika, viongozi wa dini,wanavyuo, pia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

Mtindo uliotumika, kila kundi kijinsia na umri lilipewa faragha yake, wakihofu kuwachanganya kungewanyima uhuru, vijana kuwaogopa wazee kueleza yao na wazee wakisita kunena mbele ya vijana wao, vivyo hivyo wake kwa waume katika changamoto za malezi walio nayo kwa ujumla.

Kupitia mbinu hizo, wadau wa Maria Stopes walipokutana na makundi husika, waligawanywa kijinsia kila kundi peke yake, mfano vijana wa kike walikaa kundi lao na siku walipokutana na wazazi. Kinamama walikaa kivyao, wajieleze wa kina pasipo kubughudhiwa.

Midahalo hiyo imefanyika chini ya miti yenye upepo na baridi asubuhi, wakijimuika kwa duara, pakitajwa ndiko hutumiwa kwa mikutano ya wenyeji, faragha hiyo ikishirikisha vitengo vya umma.

Hapo kunatajwa; Mama na Mtoto hospitalini, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jamii, Polisi Dawati la Jinsia na Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Mlele, waliofika kwa nyakati na siku tofauti.

Kwa mujibu wa maofisa hao wa Maria Stopes, hatua ya kwanza ilikuwa kubaini shida, kuwaelimisha wahusika ili wasikilize changamoto zao na kuzifanyia kazi, ikiwamo kuziripoti maeneo husika.

Nipashe iliyokuwapo katika hadhira hiyo siku zote wiki iliyopita ilishuhudia viongozi walioka katika mduara wakiandika wanayoyapata na mwisho walipewa fursa ya kuelimisha na kujibu maswali ya umma, ambayo kwa kiasi kikubwa yalilenga kujua matendo yanayoangukia tafsiri ya ukatili.

Wawezeshaji wa mdahalo huo, Maria Stopes, walijigawa kwenye makundi kusikiliza yanayojiri na baada ya mdahalo kumalizika, waliwachanganya pamoja kueleza waliyoyasikia au kuambiwa na kila kundi.

**SHIDA YA ZAHANATI**

Katika kufahamishana huko, ndiko kukaibuka malalamiko ya wajawazito kutotendewa haki, mwanamama anayejitambulisha kwa jina Rosemary Alex, akitamka kwa kauli ya kusikitika:

"Zahanati yetu ya Mapili kuna changamoto, saa hizi ukienda pale mjamzito usiku kuanzia saa moja mpaka uende na mwenyekiti wa kitongoji, usipompata mwenyekiti wa kitongoji, mhudumu hatoki na hatimaye utakaa kama kujifungua utajifungulia nje."

Hapo ndipo mama huyo alipotakiwa kufafanua na kuthibitisha madai yake, pia madhila yanayowakuta. Rosemary akafafanua: "Hatoki, eti wanaogopa wanaweza wakavamiwa kwa sababu zahanati haina mlinzi...Tunakutana na madhara mengi, ikiwemo vifo vya kulazimisha na watu wapo ambao tayari wameshapoteza maisha.

"Sio kwamba naongea vya 'kubumba'(kutunga), ni kweli hiyo ipo hata Mheshimiwa Diwani analijua na alishalifikisha kwenye uongozi na hatimae wakamchukia."

Anasema, wakazi wameshaomba kujengewa kituo cha

**INAENDELEA UK.12**

MAZINGIRA

# Mradi maji, ulivyo na kasi kukabili mabadiliko ya tabianchi Simiyu



Shughuli za uhamishaji kaburi, eneo la Nyakabindi, Bariadi, zikiendelea. **PICHA:NEEMA HUSSEIN**

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HADI sasa Mradi wa Maji Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, Simiyu, maandalizi yake yanatajwa kushika kasi na hadi sasa, kuna operesheni kuhamisha maeneo ya maziko, ili kupisha eneo la bomba kuu la maji litakaloanzia Ziwa Victoria.

Kazi ya kutoa nafasi kupisha utekelezaji wa mradi huo, kwa kuhamisha maeneo ya maziko ni shirikishi na inawahusisha ndugu wa familia wa wapendwa waliohifadhiwa katika maeneo hayo, pamoja na viongozi wa serikali za mitaa.

Idadi ya makaburi 78 yanatarajiwa kuhamishwa, lakini hadi mwezi mmoja uliopita, kuna jumla ya makaburi 22 yalishahamishwa kwa kushirikisha familia husika, wakihifadhiwa katika maeneo mapya nje ya eneo la ujenzi wa bomba kuu la maji.

> **Huu mradi wa maji utakaoanzia Ziwa Victoria unaenda kutunufaisha sisi wote, pamoja na jirani zetu, ikiwemo mifugo yetu itapata maji ya kutosha.**

Mratibu wa Mradi huo, Mhandisi Mwajuma Waziri, anasema wakati kazi hiyo inaendelea, kila familia iliyoathirika na hilo inapewa 'asante' na serikali ,na endapo mabaki hayatapatikana kwa sababu yoyote, ikiwamo kukosea alama za mahali lilipo kaburi.

Anasema, hata penye mabaki yatakayopatikana, bado familia husika itapewa stahiki kama ilivyopangwa na serikali na anafafanua zaidi: "Zoezi hili lote la kuhamisha makaburi ya wakazi wa kijiji cha Itilima linagharamiwa na serikali."

Pia, Mhandisi Mwajuma, anafafanua kila kaburi litakalochimbwa, kutakuwapo timu ya wataalamu wa afya watakaokagua mabaki, ili kujiridhisha usahihi wa mabaki yatakayopatikana.

### MA-DC WAONGEA

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapanga anasema familia zinapaswa kutoa ushirikiano kwa sababu, jambo linalofanywa ni la maendeleo katika jamii na hatua ya msingi, ni familia husika kushirikiana na kuepuka malumbano yasiyo na afya katika jamii.

Pia, Mkuu wa Wilaya ya Busega, Gabriel Zacharia, anawaambia wananchi wanaohitajika kuhamisha eneo la maziko, kuwa jambo la msingi kwao ni kupokea hatua hiyo ya maendeleo kwa mikono miwili, huku akikiri ni jambo zito kifamilia, mila na utamaduni.

"Huu mradi wa maji utakaoanzia Ziwa Victoria unaenda kutunufaisha sisi wote, pamoja na jirani zetu, ikiwemo mifugo yetu itapata maji ya kutosha," anasema, akihimiza mradi utakaokuwa jibu la changamoto ya huduma ya maji kwao.

Mzee Saguda Mayenga, ni kiongozi katika moja ya familia iliyohamisha eneo la maziko, akishukuru ushirikiano unaojitokeza kati ya serikali na familia zao

Anasema, Mradi wa Maji wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, Simiyu ni kati ya mradi wa maji utakaoleta mapinduzi makubwa kwa kuwahudumia wananchi, mifugo yao na kuendeleza masuala ya kilimo.

Kwa kuzingatia athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Simiyu, serikali inatekeleza programu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi ijulikanayo kwa jina Simiyu Resilient Development Programme.

Programu hiyo ina lengo la kuwezesha jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi, hasa ukame kwa kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Wilaya zote za Bariadi, Meatu, Maswa na Itilima.

Inaelezwa hadi sasa, Wizara ya Maji, inafanikisha utekelezaji wake na awamu ya kwanza, ikiwa na thamani ya Euro milioni 171 kutoka Mfuko wa Dunia wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund) na Serikali ya Ujerumani.

Taarifa iliyoko ni kwamba utafiti wa wataalamu wa mazingira, wakiwamo wa Umoja wa Mataifa, umebainisha kuwa mabadiliko ya hali ya hewa huchukua muda mrefu, pia yanaweza kuwa ya asili.

Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1800 shughuli za kibinadamu zinatajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa, kuathiri hewa na mazingira.

Wizara ya Maji imefanya juhudi kubwa kujenga miradi ya maji kwa kupeleka huduma katika maeneo yenye changamoto.

Moja ya mradi wenye mafanikio makubwa ni mradi wa Maji wa Tabora-Igunga-Nzega ambao chanzo chake ni ziwa Victoria. Mradi huu unanufaisha zaidi ya wakazi milioni moja.

Nchini na duniani kote kwa ujumla, suala la utunzaji wa mazingira ni jambo la msingi kwa mustakabali wa maisha ya sasa na baadae, mazingira yanapoharibika sio tu binadamu anaathirika, bali viumbe wote huwa katika shaka ya maisha au kupotea kabisa kwa sababu ya uharibifu.

## Sakata wanakijiji wafunguka mkutanoni wajawazito zahanati wafungiwa

**INATOKA UK.11**

afya na kuongezewa wahudumu, ikiwemo kuwekewa mlinzi wa kudumu, maana aliyekuwepo alikuwa wa kujitolea analipwa na wananchi. Pia, anashauri wawekewe umeme katika zahanati hiyo.

Baada ya kuibuliwa hoja hiyo tata, ndipo Nipashe iliyokuwa sehemu ya hadhira ilichukua hatua kupata ufafanuzi wa kiserikali kutoka kwa Kaimu Mratibu Kitengo cha Mama wa Zahanati ya Mapili, Yuster Kayombo, kuhusu dai hilo, naye akawa na majibu:

"Hivyo, vifo vya kinamama na watoto ni kweli vinatokea, lakini hatuna habari sahihi, kwamba ni kweli hawapokewi hawa wazazi. Hilo nimelipata hapa, lakini tutalishughulikia. Vifo vimetokea, lakini miaka ya nyuma.

"Kwa sasa hivi tumejitahidi kuboresha huduma. Sasa hivi tuna mpango wa kuongeza watoa huduma, pia maana sasa hivi tuna watoa huduma kama watatu tu kituoni. Kwa hiyo, tutajitahidi vifo visitokee.Tulibaini awali vilipokua vikitokea.

"Changamoto ilikuwa mama kutowahi kliniki kwa wakati mama anakaa mpaka miezi minane hadi tisa hajafika kliniki. Anaanza kifafa cha mimba akiwa nyumbani, mwisho wa siku analetwa hospitali akiwa amepoteza fahamu.

"Tunampokea, tunampa huduma, mwisho wa siku anapoteza maisha au saa nyingine analetwa mama ambaye tayari yupo kwenye hatua za mwisho kukata roho," anakiri Mratibu huyo.

Anaendeleza utetezi wake dhidi ya tuhuma, akisema:"Zahanati ya Mapili ni kweli haina umeme, ina sola, ila mpango wetu ni muda wowote wataletewa umeme hapo."

Diwani wa Kata ya Ilela, William Miula, anakiri kuwepo changamoto hiyo zahanati, akitaja chanzo kikuu ni upungufu wa matabibu katika zahanati, dhidi ya wingi wa wahitaji huduma kijijini akikadiria idadi yao ni kati ya wakazi 8,000 na 9,000.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mlele, Theresia Ilafay, anapotakiwa kufafanua na waandishi wa habari kuhusu adha hiyo ya Zahanati ya Mpili na dai la mkasa wajawazito kudhurika au kupoteza maisha, anakana akiwa na maelezo ya kuhitimisha:

"Suala la kupoteza maisha kwa Halmashauri ya Mlele halipo, kwa sababu mpaka sasa hakuna kinamama ambao wamepoteza maisha kwa mwaka wa fedha uliopita. Kikubwa serikali iliiona hilo na ni ajenda ya serikali kuhakikisha inajali wataalamu.

"Hivi juzi tu kama wiki mbili (sasa wiki tatu) zimepita, tumepokea wataalamu ambao tutawaleta, pia katika hii zahanati ya Mapili na zahanati zingine, kwa hiyo tumepokea zaidi ya wataalamu 50..."

AFYA

KILICHOJIRI ZIARA YA MARIA STOPES

# .... Mkutano wa kijijini ulivyoanika siri utitiri wa mimba katika wilaya

**Na Neema Hussein, aliyekuwa Mlele**

SUALA la kuwepo mimba kupindukia, tena kwa watoto wadogo ni ajenda inayoifikisha asasi Maria Stopes, wilayani Mlele, mkoani Katavi, hata wakakusanywa kwa wito wakazi kijijini Mapili kutaka kujua 'kisa na mkasa' nyuma ya pazia.

Ni aina ya mdahalo ambao staili yake kuu ilikuwa kutoa fursa wahusika waseme ya moyoni na wadau wote waliobaki, kuanzia viongozi wa kiserikali, hadi waratibu, wakiwa Maria Stopes, wanarekebisha na kutoa ufafanuzi, pia majibu stahiki.

Ilikuwa mwanzo wa wiki iliyopita, muwezeshaji wa asasi hiyo, Joynetha Saria, anaupa mkusanyiko wa kinamama wazazi swali la kutegua kikohozi cha siri iliyoko, akihoji mkutanoni; kinamama zamani waliishi vipi na wazazi wao waliwaambia nini kabla hawajaolewa?

Hapo ndipo akapatiwa jibu na mama anayejitambulisha kwa jina Gaudensia: "Sisi zamani tulikuwa hatutoki nyumbani bila ya kuaga. Tulikuwa tukitoka, tunaambiwa tuwahi kurudi, disko tulikua hatulijui na mavazi yetu hayakua kama haya ya sasa hivi."

Anaendelea "Kwanza tulikua tunaambiwa tusifanye mapenzi kabla ya kuolewa, kama mimi niliishi na bibi yangu aliniambia ukipata mwanaume mlete nyumbani, ili akuoe...."

Ni hoja, iliyodakwa na kuendelezwa na Rosemary Alex, akiwafunda wazazi wenzake kwamba kwao ilikuwa kawaida binti anaolewa pasipo kumjua mwanaume na anafafanua ulinganifu na kinachojiri sasa, akiwa na kitendawili chake :

"Watoto wetu siku hizi wametushinda, jamani tuseme tu ukweli! Mtoto sasa hivi anatoka ndani amevaa taiti na ameachia na mzazi upo wala husemi chochote unategemea huyo mtoto asipate mimba?"

Hapo ndipo mjadala huo wa kinamama wazazi ukachukua sura zaidi, mzazi mwingine akidakia: "Mimi siwezi kumwambia mwanangu atumie kondomu, mmh! Naanzaje sasa? Si ndio atajua namwambia akafanye kabisa, hapana!"

Katika hatua hiyo mada imekuwa juu, Muwezeshaji Joynetha, akaingilia kati akiwapa kinamama mbinu anayoitamka "ni bora kumwambia ukweli, kuliko kuwaficha, kwani wanajua kila kitu!

"Mnapowaficha, wenzenu wakienda huko nje wanafanya na wengine wanapata matatizo, bora umwambie mwanangu sikwambii ufanye ila ikitokea umefanya tumia kinga."



Wazazi wa kike walipokuwa katika mdahalo. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**





Katikati ni Kaimu Mratibu wa Kitengo cha Mama na Mtoto wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, akitoa elimu ya afya ya uzazi kwa wazazi wa kike na kiume (hawapo pichani).

### WAFUNGUKA MMOJA MMOJA

Baada ya mdahalo huo, Nipashe ikazungumza na mzazi mmoja mmoja kupata undani wa mimba hizo za watoto wa Mlele. Mama Sabina Justin, mzaliwa wa kijiji cha Mapili, anakiri kushuhudia na kusikia mimba nyingi za watoto mahali hapo.

Anaendelea kwa kutaja sababu kuu ni makundi ya vijana wanaomiliki simu za kisasa, zinaziwafikisha katika hatua ya kupekua makubwa yasiyoendana na umri wao.

"Tunaendelea kuwaelimisha watoto wetu, pia kuwapa elimu angalau kama mtu unashindwa kujizuia bora utumie kondomu, sababu usipotumia utabeba mimba ukiwa mtoto mdogo, utashindwa kuzaa utafanyiwa oparesheni," anaeleza Sabina.

Anasema imekuwa kawaida mabinti zao wanapobeba mimba, wanaume wao huwakemea, hivyo jukumu linamuangukia mama anayemlea mtoto.

"Tunajikuta tunakaa na watoto na wajukuu, kama hela ulikuwa umeandaa ufanyie mambo yako, ndio inakuwa ya kufanyia malezi hadi gharama za kujifungua, kama amefanyiwa oparesheni wewe ndio ulipie," anaeleza.

Sabina anasimulia mikasa katika familia inawaangukia tena kinamama wanapokejeliwa na waume zao hawajui kulea hadi kusababisha hizo mimba. Mwanamama Felster Masansa, anaangukia majuto akitamka: "Hiki kijiji mtoto wa miaka 12 na11 anakuwa na mimba, unapomshauri wewe mzazi hakuelewi, akishatoka anatoka na zake, siku mbili tatu unashitukia ana mimba, kuja kuzaa mtoto anazaa mtoto mwenzie.

"Chanzo chake watoto wameshakosa adabu, kutoelewa sisi wazazi, wala kutusikiliza...hamna akishaenda kuangalia kwenye video, anachukua mambo ya kwenye video, ndio anakuwa nayo.

"Elimu tunayompa kuwa mimi nilitokea hivi kwa wazazi wangu walikua wananieleza hivi, sielewekі. Anakuwa anaelewa tu ya kwake anayojua yeye, unashitukia amezaa na kumfukuza inashindikana, unarudi tena unaanza kumlea yeye, unalea mtoto tena.

"Mtoto atakapoharibika unakosa raha wewe mzazi, pale kuanzia kwa mume wako uliyekuwa naye, anasema 'akili zote amezichota kwako wewe mama yake' huna elimu ya kutosha ya kumpa mtoto.

> **Tunaendelea kuwaelimisha watoto wetu, pia kuwapa elimu angalau kama mtu unashindwa kujizuia bora utumie kondomu, sababu usipotumia utabeba mimba ukiwa mtoto mdogo, utashindwa kuzaa utafanyiwa oparesheni.**

Umeacha amezaa, yaani unakuwa unatukanwa mara kwa mara wewe mke wake, unatukanwa wewe anatukanwa na mtoto."

Mzazi wa kiume, Katawa John, alipotakiwa kufafanua mada ya mimba, anaungana na sehemu ya hoja ya Mama Sabina dhana ya simu, akiutaja utandawazi ni chanzo kikubwa, hata vijana wakawa na uhuru uliopitiliza."

Hata hivyo, mkutanoni kada ya vijana walipohojiwa kulikoni wanaangukia mimba, kwa kiasi kikubwa wakafafanua ni kutoshirikishwa kwenye vikao mbalimbali, pia wanalalamika kondomu haziuzwi kijijini.

Mzazi mwingine wa kiume, anayejitambulisha kwa jina moja la Ernest, anaiambia Nipashe akiwa na hoja hiyo, akiwa na madai mzizi mkubwa wa tatizo hilo uko kwenye kupotoka mila na desturi, akitaja zama za kale vijana walifundwa. Anarejea maisha ya kale, walipata muda wa kukaa na babu zao walipowaelimisha mengi kuhusu usalama na maadili yao ya asili, lakini sasa kuna kukinzana kwa mila, vijana wakiacha ya asili na kukumbatia ya kigeni.

### DED AKANA

"Mimi siwezi kukubaliana na hilo kwamba mimba za utotoni katika kijiji hiki ziko 400 hapana hizo data inabidi tuziangalie vizuri," Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Mlele, Theresia Ilafay, anaeleza, pale alipotakiwa kufafanua undani wa dai hilo.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa marejeo yaliyotolewa na Mratibu Ustawi Jamii wa Halmashauri hiyo, Yuster Kayombo katika mjadala kupata ufafanuzi kutoka kwa wakazi wa kijiji hicho.

Huku akitanguliza tabasamu, Theresia anafafanua kwamba hadi sasa wanapambana kupiga vita ukatili na hasa mimba za utotoni katika halmashauri yao, wakiimarisha kamati husika za wilaya, mitaa na vijiji, kuhakikisha zinatekeleza majukumu wamayopewa.

MAZINGIRA

MKUTANO WA WABUNGE VS WANAHARAKATI

# Uhaba wa matundu vyoo kwa vijana, unavyowaibulia madhila kijinsia shule

- Wanasiasa kinamama wapokea, kulishikia 'bango'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTANDAO wa Kijinsia Tanzania (TGNP), umekuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu kwa jamii, kuchukua hatua kukabili matukio yanayoshamiri nchini kila kukicha.

Ni ukatili unaodaiwa kuongezeka kwa kasi, kutokana na sababu mbalimbali katika jamii, hata kuamua kuunda vikundi vya sauti ya jamii ambavyo vimekuwa vikijihusha na kubaini sababu za kuongezeka matukio hasi kwa jinsia, kwa wanawake na watoto.

Wadau wa jinsia nchini, wanasema kuwa uhaba wa matundu ya vyoo katika shule nyingi nchini unachangia vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwemo vijana kunajisiana.



Vyoo vya shule katika sura tofauti, vilivyokamilika na vilivyo katika hatua ya ujenzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**WANAHARAKATI**

Mwenyekiti wa Sauti ya Jamii Kipunguni mkoani Dar es Salaam, Fatma Talib, akizungumza kwenye mkutano wa mashauriano kati ya wabunge wanawake na wabunge vinara wa jinsia kuhusu masuala ya kibajeti, anadai uhaba wa matundu ya vyoo, ni sababu kubwa kwa watoto shule kunajisiana.

Mkutano huo uliofanyika bungeni jijini hapa kwenye Ukumbi wa Msekwa, pia una lengo la kuishauri serikali kuwa na bajeti yenye mlengo wa kijinsia, ili kujibu kero mbalimbali zinazowakabili wanawake na watoto nchini.

Talib analalamika katika wilaya ya Ilala anakotoka, kero ya uhaba wa matundu ya vyoo katika shule za msingi imekuwa ikichangia ukatili wa kijinsia miongoni mwao.

"Unakuta tundu moja la choo linatumiwa na watoto hata 200, hivyo ule msongamano unasababisha vitendo vya kunajisiana kwa watoto katika shule zetu.

"Kuna shule moja kule kwangu, matukio ya kunajisiana kwa watoto na kufanyiana vitendo visivyokuwa vya kimaadili yalitokea na hii yote ilikuwa ni kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo hivyo, kusababisha msongamano wa watoto katika maeneo ya vyooni," anasema Talib.

Pia, anafafanua idadi ndogo ya matundu ya vyoo katika shule hiyo, imekuwa kero kwa wasichana hasa wanapokuwa katika kipindi chao cha hedhi kukosa eneo la kwenda kujisitiri.

"Watoto wa kike wanapata shida sana hasa wanapokuwa katika hedhi kwa kukosa eneo la kwenda kujisitiri kutokana na shule kutokuwa na matundu ya vyoo ya kutosha, lakini hakuna vyumba vya kujisitiri, wala huduma ya maji hali inayosababisha wakose masomo kwa zaidi ya siku 100 kwa mwaka," anasema

Vilevile, anashauri kutokana na hali hiyo, serikali inapaswa kuanza kutenga bajeti ya kijinsia, inayosaidia shule nyingi kuwa na vyumba kwa ajili ya mabinti kujisitiri wakati wa hedhi zao.

> **Kurudishwa kwa huduma za 'PF3' (za polisi) za zamani na ziwe wazi kulinda ushahidi na kuwe na usiri wa ushahidi wa madaktari, kudhibiti rushwa kwa polisi na madaktari.**




"Tunashukuru kwa fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, lakini sasa ipo haja ya kuanza kujenga vyumba kwa ajili ya mabinti zetu kujisitiri lakini pia huduma ya maji ni muhimu sana katika shule zetu hivi sasa watoto wanakwenda na vidumu vya maji shuleni," anasema.

Kwangu Limbu, kutoka wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, anasema katika kijiji cha Kiloleli anakotoka wanakabiliwa na kero kubwa ya ukosefu wa huduma ya maji hali inayosababisha watoto wengi kuacha shule.

"Tunaiomba serikali ituangalie wakati inapopanga bajeti yake sisi maji tunayapata umbali zaidi ya kilomita 15 na siyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu .

" Kwakuwa tunafuata mbali, tunalazimika kutoka majumbani saa mbili usiku na kurudi asubuhi, hali hii inasababisha watoto kuacha shule na sisi ndoa zetu kuvunjika," anaeleza.

Katika hilo, anadokeza kuwa inachangia kukwamisha shughuli za uzalishaji mali unashuka kutokana na watu kutumia muda mrefu kusaka maji.

**MTAALAMU TGNP**

Deogratius Temba, Muwezeshaji kutoka TGNP, anaishauri serikali kuongeza kiasi cha ruzuku ya kila mwanafunzi kutoka Sh. 10,000 ya sasa hadi Sh. 25,000 kwa mwaka .

Anasema ni kiasi kitakachosaidia shule kujiendesha na kuwezesha huduma mbalimbali kwa wanafunzi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mbinti taulo za kike. Kiasi cha Sh. 10,000 ni kidogo sana kimekuwa kikitumika kwa zaidi ya miaka 20.

"Sasa ni wakati mwafaka kuongeza hadi Sh. 25,000, ili kukidhi hali ya mabadiliko ya uchumi kwa sasa na kusaidia kutoa huduma kwa wanafunzi za uji pamoja na taulo za kike ili watoto washiriki masomo bila kukosa," anasema Temba.

Vilevile, anaishauri serikali kuandaa mwogozo wa bajeti ambao utazilazimisha halmashauri zote nchini kuwa na bajeti zenye mlengo wa kijinsia ili kutoa taulo za kike kwa wanafunzi pamoja na kuandaa vyumba vya kujihifadhia mabinti wanapokuwa katika hedhi.

"Mapendekezo yetu katika sekta ya elimu kila mwaka serikali kuu ilipe kipaumbele suala la ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari za kata. Tunaomba sana kila mwaka yajengwe mabweni," anasema.

Temba anashauri kuwepo maji ya kutosha shuleni, ili kuwasaidia watoto wa kike hasa wakiwa katika siku zao, kuongezwa matundu ya vyoo, bajeti ya taulo za kike itengwe na iwe ya lazima.

"Tunaiomba serikali kuu itoe maelekezo kwa halmashauri zote kutenga bajeti ya taulo. Hili linawezekana, kwa sababu kuna halmashauri hazina mapato makubwa lakini zimeweka bajeti hiyo.

"Mwongozo wa bajeti ya serikali, utoe maelekezo ya kuwepo kwa bajeti ya taulo, ramani za ujenzi wa matundu ya vyoo kwa shule zote iwe moja na ielekeze uwepo wa vyumba maalum kwa ajili ya wasichana wakati wa hedhi," anasisitiza Temba

Pia, anafafanua kwa wao TGNP wana pendekezo lao katika kupunguzwa ukatili wa kijinsia, wakitaka kuanzishwa madawati ya jinsia ngazi ya shule na ofisi ya kata.

"Kurudishwa kwa huduma za 'PF3' (za polisi) za zamani na ziwe wazi kulinda ushahidi na kuwe na usiri wa ushahidi wa madaktari, kudhibiti rushwa kwa polisi na madaktari," anasema.

**WABUNGE KINAMAMA**

Mwenyekiti wa chama cha Wabunge wanawake, Magreth Sitta, anasema yote yaliyowasilishwa kwao na wanajamii hao, watabeba na kuishauri serikali kuyafanyia kazi.

"Pia ninawashauri kuwa, mambo ya bajeti pia wanapaswa kuzishauri halmashauri zao, kwa sababu hivi sasa hii bajeti kuu inaposomwa, inakuwa tayari imeshamaliza kila kitu," anasema Mama Sitta.



# DC awaonya wadahili makarani sensa kupokea rushwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewaonya waratibu elimu na wakuu wa shule za sekondari na msingi za serikali katika Jiji la Dodoma waliopewa dhamana ya kudahili makarani wa Sensa ya Watu na Makazi, kujiepusha na vitendo vya kupokea rushwa na kufanya upendeleo.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu huyo wa wilaya alipokuwa akifungua semina ya kuwaandaa waratibu na walimu hao kwa ajili ya udahili kwa watakao andikisha sensa ya watu na makazi wa jijini hapo.

Akizungumza kwenye semina hiyo, Shekimweri aliwataka wafanye kazi hiyo kwa weledi mkubwa na sio kupokea vimemo vinavyoashiria vitendo vya rushwa na upendeleo au kuangalia sura badala ya sifa husika.

"Ninawasihi nyinyi mnaoenda kuwafanyia udahili makarani msijivunjie heshima zetu kwa kupokea rushwa ya shilingi elfu tano, kumi au 100,000 na mkapoteza sifa zenu, naombeni mkatumie mwongozo uliotolewa ili muweze kuwapata makarani hao wenye sifa.

"Nawaomba sana jambo hili lifanywe kwa miongozo na vigezo na kwa weledi mkubwa mno huku pia mkiwa wasiri kwenye kufanya kazi hiyo wakati wa kuwasajili makarani hao," alisema.

Alisema wapo watu watakaodiriki kupenyeza vimemo kwenu ili waweze kuwaingiza ndugu zao kwa njia hiyo na taifa likashindwa kufikia malengo yake ya uandikishaji wa sensa ya watu na makazi.

Kadhalika, aliwataka kujitambua kwa kuwa wao wameaminiwa na wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii na uaminifu mkubwa.

Aliwataka wahakikishe wanahamasisha kwa kupitia makundi mbalimbali yakiwamo wanamichezo, wacheza ngoma, wasanii, wachoraji, waimba kwaya, watunga mashairi na ngonjera ili sensa ya watu na makazi iweze kufanikiwa.

Vilevile, aliwataka wakawe mabalozi wa kukemea wale wote wanaopotosha kuhusu suala la sensa kuwa halifai bali wakawaelimishe kuwa zoezi hilo lipo kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania wote.

Kwa upande wake, Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi wa Jiji la Dodoma, Calista Makacha, aliwataka wasahili hao kutunza siri kama sheria ya takwimu inavyosema huku wakizingatia vigezo vya kuwapata makarani wanaotakiwa.

Pia, aliwataka kuzingatia vigezo na kuacha kupokea vimemo vinavyoweza kuwaondolea sifa na wakawe wazalendo wakati wote watakapofanya usahili huo kwa makarani.

# RUWASA kukamilisha mradi bwawa kunyweshea mifugo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), unatarajia kukamilisha mradi wa maji na bwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo kwenye Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mwishoni mwa mwezi Julai, mwaka huu.

Kijiji hicho kilikumbwa na uhitaji wa maji baada ya wananchi kutoka Ngorongoro waliohamia eneo hilo kwa hiari. Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, akizungumza juzi na waandishi wa habari, alisema RUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji hicho na mpango wa utekelezaji uligawanywa katika awamu mbili.

Alisema awamu ya muda mfupi imekamilika na vituo vya kuchotea maji 12 vimeshaanza kutoa huduma ya maji.

"Awamu ya pili imefikia asilimia 70 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2022. Kukamilika kwa awamu hiyo kutawezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 17,000 pamoja na mifugo yao na kufanya idadi ya vituo vya maji kuongezeka kutoka 12 hadi kufikia vituo vya kuchotea maji 30 kwa matumizi ya binadamu na vituo tatu vya kunyweshea maji mifugo," alisema.

Aidha, alisema kuboresha huduma ya maji katika Kijiji cha Msomera, serikali kupitia RUWASA inaendelea na ujenzi wa bwawa la maji kwa gharama ya Sh. bilioni 1.99 na kwa sasa umefikia asilimia 15.

"Ujenzi wa bwawa hili utakapokamilika, utasaidia kuboresha huduma ya maji kwa wananchi na mifugo yao pia," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza na wakazi wa kijiji cha Mtera, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani humo mapema wiki hii, alipokwenda kukagua ujenzi wa mradi wa maji unaotekelezwa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TFRA yaweka mfumo imara utoaji mbolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imesema katika msimu ujao wa kilimo imeweka mfumo imara wa utoaji mbolea ya ruzuku kwa wakulima ambao hautakuwa na mianya ya ubadhirifu.

Akizungumza katika kipindi cha Kumepambazuka cha Redio One, Mkurugenzi wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alisema hatua hiyo inalenga kuondoa kero zilizojitokeza katika mifumo ya ruzuku iliyopita.

"Serikali imeandaa mfumo wa kielektroniki ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa kuziba mianya ya ubadhirifu ili mbolea ya ruzuku iweze kuwafikia wakulima ambao ndiyo walengwa," alisema Dk. Ngailo.

Alifafanua kuwa ili kuhakikisha wakulima wananufaika serikali imejiwekea mfumo imara na bora wa utoaji wa ruzuku za mbolea ambao utasaidia kuwafikia wakulima.

Dk. Ngailo alisisitiza kuwa katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika mifumo ya ruzuku iliyopita serikali imeandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa waingizaji, wasambazaji, wauzaji wa mbolea

pamoja na wakulima wanaotarajiwa kunufaika na mbolea hizo za ruzuku.

Alisema kuwa mfumo huo utatumika katika kuhakikisha huduma zote za usambazaji wa mbolea za ruzuku unatolewa na mtu sahihi na kumfikia mkulima mwenyewe na si vinginevyo.

"Serikali imejipanga kuhakikisha mfumo huo unafanya kazi kwa ufasaha ili mkulima aweze kunufaika na ruzuku ya mbolea ambayo inatolewa," alisema Dk. Ngailo.

Akizungumzia namna usajili utakavyofanyika Dk. Ngailo alisema usajili utafanywa na ofisa ugani waliopo katika ngazi za kata na vijiji na kuthibitishwa na mwenyekiti wa kijiji na baadaye taarifa za mkulima kuingizwa katika mfumo wa kielektroniki ili kuwezesha usambazaji wa mbolea hizo.

Aliongeza kuwa mzalishaji au mwingizaji wa mbolea nchini atatumia mifuko maalum kwa ajili ya ruzuku yenye QR code na maandishi yanayosomeka ili kuutambulisha kuwa mbolea hiyo inanunuliwa na mkulima kwa bei ya ruzuku.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Uingizaji wa mbolea kwa pamoja kutoka TFRA, Elizabeth Bole, alisema utoaji wa ruzuku za mbolea sio jambo jipya nchini isipokuwa serikali imeendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa mbolea hizo ili kuondoa mianya ya ubadhirifu ikiwamo kusaidia wakulima waweze kunufaika na ruzuku hiyo.

Bole alibainisha kuwa mnufaika wa mbolea ya ruzuku ni aliyesajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa ruzuku ambao mkulima atasajiliwa kwa jina, kijiji anachoishi, ukubwa wa eneo la shamba na kutoa picha halisi ya kiasi cha mbolea kinachohitajika kwa ajili ya shamba lake.

Kadhalika, alisema utoaji wa ruzuku za mbolea ni matokeo ya maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuona umuhimu wa kuwawezesha wakulima kulima kwa tija.

Alisema Sh. bilioni 150 za kitanzania zimetengwa ili kutumika kutoa mbolea za ruzuku kwa wakulima kwa mwaka wa fedha 2022/2023.





# Wakulima wamgomea DC kuachia eneo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO umeibuka kati ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua na wakulima wa skimu ya umwagiliaji ya Bonde la Uyole jijini Mbeya kutokana na kiongozi huyo kuwataka wananchi hao waiombe serikali waendelee kulitumia eneo hilo.

Skimu hiyo inatumiwa na zaidi ya wakulima 1,500 ambao wanazalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya bustani, lakini eneo hilo linaelezwa kuwa ni mali ya Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya huku wakulima nao wakidai ni lao.

Inaelezwa kuwa hospitali hiyo inataka kuanza kuliendeleza eneo hilo kwa kujenga baadhi ya miundombinu ikiwamo ya kitengo cha magonjwa ya saratani lakini wananchi wanadai hawako tayari kupisha eneo hilo wakisisitiza kuwa ni mali yao.

Kutokana na mvutano huo, Dk. Chuachua alitembelea eneo hilo na kuwataka wakulima hao kuandika barua ya kuiomba serikali iwaruhusu waendelee kulima au wapishe kwa ajili ya matumizi ya hospitali.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika juzi kwenye eneo hilo, wakulima hao walisema hawako tayari kupisha eneo hilo wala kuiomba serikali kwa maelezo kuwa eneo ni mali yao na wanamiliki kihalali.

Mwenyekiti wa Skimu hiyo, Maneno George, alisema viongozi wa hospitali wamekuwa wakiwaeleza kwamba eneo hilo ni mali yao, lakini wakiwauliza walilipata katika mazingira gani, wamekuwa wakikosa majibu.

Alisema eneo hilo ni mali ya wakulima kwa asili lakini hivi karibuni waliambiwa na uongozi wa hospitali kuwa taasisi hiyo inalimiliki tangu mwaka 1976.

Baada ya kuwakatalia viongozi wa hospitali hiyo, ndipo wakaamua kwenda kushtaki kwa mkuu wa wilaya ambaye aliwataka wakulima hao kuondoka kwenye mashamba hayo.

"Walipokwenda kwa mkuu wa wilaya ndiyo maana na yeye akaja hapa na kutuambia kwamba tumechukua eneo la watu, lakini hatujui misingi hasa ya kusema eneo ni la kwao," alisema Maneno.

Diwani wa Iganjo, Eliud Mbogela, aliwahoji wananchi hao kama wako tayari kuandika barua ya kuiomba serikali iwaruhusu kuendelea kulitumia eneo hilo, ndipo wakaitikia kwamba hawako tayari.

Alisema hawaoni sababu yoyote ya msingi ya kuandika barua ya kuomba eneo lao na badala yake wanamtaka mkuu huyo wa wilaya aende akazungumze nao akiwa ameambatana na viongozi wa hospitali ili mmiliki halali ajulikane.

Alimtaka mwenyekiti wa skimu hiyo kumpelekea mkuu wa wilaya majibu ya wananchi kwamba wanamhitaji yeye mwenyewe aende akawaambie kuhusu kuomba eneo hilo ambalo wanalimiliki.

Baadhi ya wakulima walisema agizo la mkuu wa wilaya linalenga kuwasababishia njaa kwa maelezo kuwa wanalitegemea eneo hilo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na kwamba hata uchumi wao unatokana na mashamba hayo.

Mmoja wa wakulima hao, Agnes Mengo, alisema mkuu huyo wa wilaya analenga kuwaua, hivyo hawako tayari kuondoka na kwamba hata kama nguvu itatumika, hawako tayari kuondoka.

Dk. Chuachua alisema lengo la kuwataka waiandikie serikali barua ni kutaka waombe kuendelea kulitumia ili hospitali ipewe eneo lingine.

Alisema eneo hilo linatumiwa na wakulima wengi ambao wamewekeza nguvu na fedha zao kwenye ujenzi wa mifereji na kuyahudumia mashamba hayo.




Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi (kushoto) akipokea picha ya Ziwa Ngosi kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, wakati wa kikao cha wadau wa utalii jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maandalizi sensa watu, makazi yapamba moto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAALAMU wa Sensa ya Watu na Makazi wanaotarajiwa kwenda katika halmashauri mbalimbali za mkoa wa Mbeya kuwafundisha makarani wa sensa hiyo, wameanza mafunzo ya kujaribu vifaa ili kuona kama vinafanya kazi sawasawa.

Moja ya majukumu wanayofanya ni pamoja na kuvitumia vifaa hivyo hasa vishikwambi kutambua mipaka ya mitaa, vijiji na vitongoji wakati wa kuhesabu watu ili kuepuka makarani kuingiliana wakati wa suala hilo Agosti 23, mwaka huu.

Vilevile maofisa hao wanafanya majaribio ya kukusanya takwimu mbalimbali za baadhi ya kaya, huduma za kijamii pamoja na taasisi mbalimbali zinazopatikana kwenye makazi ya watu.

Wataalamu hao walianza kazi hiyo ya kujaribisha vifaa juzi kwa kufanya majaribio kwenye kata tano ambapo walifanya majaribio kwenye kata moja ya vijijini ambayo ni Iwindi iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kata nne za Jiji la Mbeya.

Mratibu wa Sensa wa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa, alisema jana kuwa maofisa hao wamefundishwa namna ya kuvitumia vifaa hivyo katika mazingira ya aina yoyote, hivyo majaribio wanayofanya ni kutaka kuangalia vile ambavyo vina hitilafu viondolewe na viletwe vingine.

Alisema mfumo huo mpya utasaidia kukusanya takwimu zote zinazohitajika kwa wakati na kupunguza gharama za uendeshaji pamoja na muda.

Alisema kwenye sensa kuna vitu muhimu ambavyo serikali inalenga kuvibaini ikiwamo nguvu kazi ya taifa kwa kuangalia umri wa Watanzania, idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule, idadi ya watu wenye mahitaji maalumu pamoja na kuangalia idadi ya watu waliofikia umri wa utegemezi.

"Sensa ni zoezi muhimu kwa taifa lolote hasa wakati wa kupanga mikakati mbalimbali ya maendeleo, tukijua idadi ya watu inakuwa rahisi serikali kuwahudumia watu wake kwa kuwapelekea huduma mbalimbali," alisema Lyakurwa.

Alisema katika mkoa wa Mbeya, maofisa walioshiriki mafunzo hayo wako 300 na kwamba watasambazwa katika halmashauri zote za mkoa kwenda kutoa elimu kwa makarani.

Alisema wakati wakimaliza mafunzo hao kwa wataalamu hao, usaili unaendelea wa kuwapata makarani wa sensa na kwamba mkoa mzima utakuwa na zaidi ya makarani 7,000.

Aliwataka viongozi serikali katika maeneo mbalimbali ya mkoa, kushiriki katika k uwahamasisha wananchi kushiriki sensa ili kupata takwimu sahihi.

## Mbunge awataka wazazi kuwapeleka watoto shule

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MBUNGE wa Lupa wilayani Chunya, Masache Kasaka, amewataka wazazi na walezi kuendelea kuwapaleka watoto wao shule kutokana na serikali kupunguza gharama za elimu katika ngazi zote.

Aliyasema hayo katika maeneo mbalimbali ya jimbo alikofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi huku akisema kwa sasa serikali imeondoa ada kuanzia darasa la awali mpaka kidato cha sita huku ikiongeza bajeti ya kuwakopesha wanafunzi wa vyuo vikuu.

Vilevile alisema serikali imeboresha miundombinu ya elimu kwa kutumia fedha zinazotokana na vyanzo mbalimbali na hivyo hakuna sababu ya mzazi kutompeleka mtoto wake shuleni.

Kasaka alisema vitendo vya wazazi kutowapeleka watoto shuleni vinasababisha ongezeko la ndoa za utotoni, mimba za utotoni pamoja na ongezeko la ajira za watoto kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

"Huku kwetu kuna shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, tunachimba madini, tunalima tumbaku na wengine tunafuga, sasa usipompeleka mtoto shule ni kwamba tafsiri yake unataka aje afanye hizi kazi jambo ambalo sio sahihi kisheria," alisema Masache.

Vilevile aliwataka wazazi kushiriki katika kuboresha miundombinu ya elimu badala ya kuiachia serikali pekee ifanye kazi hiyo kwa maelezo kuwa mzigo unakuwa mkubwa.



## HABARI ZANZIBAR

# Rais Mwinyi ampongeza mwekezaji hoteli kuajiri 350

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amempongeza mwekezaji wa Hoteli ya RUI Jambo iliyoko Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa imani kubwa alionyesha na kufanikisha uwekezaji wa mradi mkubwa wa hoteli ya kitalii.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika uzinduzi wa hoteli hiyo, hafla iliyofanyika Nungwi, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kutembelea miradi mbalimbali katika mikoa ya Unguja na Pemba, ikiwamo inayoendelezwa kupitia fedha za ahueni ya UVIKO-19.

Alisema hatua ya mwekezaji huyo kuwekeza hoteli kubwa ya nyota nne, imewajengea imani wawekezaji wengine kuja kuwekeza nchini katika miradi mikubwa.

Dk. Mwinyi alipongeza Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), kwa utendaji kazi mzuri na kuitaka taasisi hiyo kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Alisema kukamilika kwa hoteli hiyo kutawawezesha Wazanzibari kunufaika ipasavyo na ajira na kubainisha kuwa Watanzania wapatao 350 wameajiriwa hotelini hapo. Aidha, alimpongeza mwekezaji huyo kwa kutoa ajira kwa wananchi sambamba na kununua bidhaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya hoteli kutoka hapa nchini, ikiwamo bidhaa za kilimo pamoja na uvuvi na kutoa fursa kwa wananchi hao ya kujiongezea kipato.

Dk. Mwinyi, alisema hoteli hiyo imekuwa ikiitangaza Zanzibar kimataifa, hatua itakayochochea ujio wa watalii wengi nchi ni. Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alisema serikali imejizatiti kuja na mradi mkubwa wa maji wa uhakika katika maeneo hayo, ili wananchi na wawekezaji wapate huduma hiyo kwa uhakika.

Katika utekelezaji wa jambo hilo, Dk. Mwinyi aliwataka wananchi kuwa walinzi wa miundombinu ya maji, huku akibainisha kuwapo wananchi wanaoharibu kwa makusudi miundombinu hiyo ili kupata fursa ya kupeleka maji katika hoteli kwa njia ya magari na kujiingizia kipato.

Alisema serikali ina mpango wa kuleta vifaa vipya na vya kisasa vya upakuzi wa mizigo bandarini, ikiwa ni juhudi za kuharakisha kazi za kupakua mizigo, ikiwamo ya wawekezaji.

Hata hivyo, aliwataka vijana wanaotembeza wageni 'Beach Boys' kujiandaa kwenda katika maeneo maalum yanayotayarishwa kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa mbalimbali za ujasiriamali, ikiwa ni hatua ya kuondoa bughudha kwa watalii.

Naye, Waziri wa Uwezeshaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema katika kipindi cha awamu ya nane, chini ya uongozi wa Dk. Mwinyi, nchi imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuvutia wawekezaji, kiasi ambacho wale waliokuwa wamekata tamaa wameanza kuja kuwekeza na kuipongeza ZIPA kwa utendaji uliotukuka.

Waziri wa Utali na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, alimtaka kila Mzanzibari kuwa balozi katika uimarishaji wa sekta hiyo ili kutangaza na kuvutia watalii kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa.

Kwa upande wake mwekezaji wa hoteli hiyo, Carlos alisema hoteli hiyo ina azma ya kuwafanya wafanyakazi, wana jamii na wananchi wanaotoa huduma mbalimbali katika hoteli hiyo kufurahia na uwapo wake.

Hoteli ya RUI Jambo ina jumla ya vyumba 461 na itakapokamilika itakuwa na 1000, ikiwa tayari imetumia Dola milioni 61 na kutoa ajira 368.

## Watendaji watakiwa kuwajibika kero za wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi, amewataka watendaji wa wizara hiyo kuwajibika wanapo wahudumia wananchi maji, nishati madini ili kuwaondolea kero inayowakabili.

Aliyasema hayo mjini hapo, wakati akizungumza na watendaji hao kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa wizara anayoisimamia ili kupunguza malalamiko ya huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Alisema maji yanaweza kupatikana, lakini anashangazwa watu hawapati maji huenda kuna watu wanafunga maji kwa makusudi ili watumie magari kwa ajili ya kufanya biashara ya maji huku wananchi wakiteseka jambo ambalo sio sahihi.

Aidha, aliwataka watendaji hao kila mmoja kuwajibika katika majukumu aliyopewa bila ya kusubiri kuwajibishwa kwa sababu kila mfanyakazi anapewa majukumu yake.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji, kufunga mfumo wa alama za zidole haraka iwezekanavyo ili kuangalia kwa karibu mahudhurio ya wafanyakazi na kudumisha nidhamu ya kazi.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mwanajuma Majid Abdalla, alisema endapo wananchi hawapati huduma ya maji, wizara itakuwa haina uwajibikaji ikizingatiwa kuwa huduma hiyo ni muhimu.



Waziri wa Jinsia, Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akitunza pesa kwa wacheza ngoma ya asili aina ya msewe katika sherehe za ufunguzi wa madrasa mpya ya Shule ya Msingi Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wananchi wafurahia kivuko kurahisisha upatikanaji elimu

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Shehia ya Mjini Wingwi, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, wameipongeza serikali kwa kuwajengea kivuko ambacho kimesaidia kurahisisha upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wa shehia hiyo. Walisema, wamefarijika kuona serikali inaendelea kufanya juhudi za kuwapatia huduma muhimu za kijamii ikiwamo kuwajengea daraja ambalo limesaidia watoto kuvuka bila usumbufu kufuata elimu.

Akizungumza na waandishi wa habari, mkazi wa kijiji hicho, Punje Bakar Maalim alisema, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ni mkombozi mkubwa wa wananchi hasa wanawake na imewakomboa kutoka katika hali duni za maisha yao.

Alisema, daraja hilo ambalo wananchi kwa kushirikiana na mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na TASAF limewasaidia kwa asilimia kubwa na limewaondolea usumbufu na kuwarahisishia wanafunzi kufika shule kwa wakati.

"Watoto wenye umri mdogo ambao wanasoma shule za maandalizi tulilazimika kuwabeba kuwazungusha maeneo ya mbali ili wafike shule, utoro pia ulikuwa ni mwingi katika shule zetu kutokana na usumbufu uliokuwapo," alisema.

Aidha, aliomba serikali kuwaboreshea daraja hilo badala ya kujengwa kwa miti liwe la kudumu ili kuleta manufaa zaidi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Bizume Khalfan Faki, pia mkazi wa shehia hiyo alisema, TASAF inawasaidia katika maisha yao ya kila siku tangu kuanza kwake mwaka 2005 hadi mwaka huu.

"Tuliamua wananchi tujenge daraja kutokana na watoto wetu kutoroka shule kwa ajili ya usumbufu wa kutembea masafa marefu kufuata elimu, wakati njia rahisi ipo ambayo inakaa maji mengi, kwa kushirikiana na TASAF daraja limekamilika," alisema.

Hata hivyo, alisema wananchi wa shehia hiyo hawakuwa na hamasa ya kusomesha watoto wao, lakini kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini wamehamasika kusomesha kuanzia maandalizi, msingi, sekondari na hata vyuo vikuu.

Katibu wa sheha, shehia ya Mjini Wingwi, Massoud Kombo Hassan, alisema faida nyingi zimepatikana kuwapo kwa mradi huo ikiwamo kivuko salama na kabla ya ujenzi wa daraja hilo mtoto aliwahi kupoteza maisha akivuka kupitia daraja la awali ambalo halikuwa rafiki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## WINDING UP THE COMPANY

**MWASHA JOJE COMPANY LIMITED**
**P. O. Box 14962 Dar Es Salaam,**
**Email: mwasha.a@gmail.com,**
**Tell: 0784 470615**
**Register No.123485.**

**NOTICE FOR THE GENERAL MEETING OF WINDING UP THE COMPANY.**

The final meeting will be held at registered office at kariakoo-agrey street on **1/3/2022 starting at 09:00am**

**Agenda.**
The purpose of the meeting is for determine of an account of winding up report from the liquidator.

Liquidator; **ATHUMANI JERRY MWASHA.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MBINGA.**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 68/2021.**
**MAKSENSIA MBELE ––––– MRUFANI /MUOMBAJI.**
**DHIDI YA.**
**EMMANUEL MBELE –––––MRUFANIWA /MJIBU MAOMBI.**

### WITO KUITWA SHAURINI

**MDAIWA EMMANUEL MBELE, POPOTE ULIPO.**
**BW/BI, MAKSENSIA MBELE,** amefungua shauri Mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo (Boma). Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 10/8/2022 Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mbinga.Endapo hutatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri /Muhuri wa **Baraza hili leo hii tarehe 05 mwezi wa 07 mwaka 2022.**

–––––––––––––––––––––––
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MBINGA.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**Mahakama ya Mwanzo ya KAWE**
**Wilaya ya KINONDONI**

**MADAI NAMBARI 07 YA 2022**
**Mdai: RICHARD .V. MWANSASU**
**Amdai**
**Mdaiwa KAMPUNI AMIL FINANCE LIMITED**
**Kwa: KAMPUNI AMIL FINANCE WA MWENGE – DAR ES SALAAM.**

**Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba**

**KUJIBU MADAI YA PESA TSH. 46,700,000/=**
Kwa hiyo unahitajiwa / mnahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 25/7/2022 saa 2:30 Asubuhi / Alasiri kwa kujibu madai haya. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria / hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
**Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 20/7/2022.**

MAHAKAMA YA MWANZO KAWE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**ROLL AGROVET (T) LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi ya **TRAILER** yenye usajili namba **T531 DGE na CHASSIS NAMBA: X1962000020002114.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/285837/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.103 of 2022**

**In the matter of the Estate of the late HABEL ENOCK MHEMBANO Msangalale West Street, Dodoma Makulu ward, within Dodoma City.**

**AND**

**In the matter of an application for letters of administration by GRACE ENOCK MHEMBANO and MUSA HABEL ENOCK.**

### GENERAL CITATION

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 22 Day of AUGUST 2022

Dated at Dodoma this 19 day of 07,2022

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:
SMMN CITY ATTORNEYS (ADVOCATES)
Plot No.96, Block V
Baruti Street, near Airport Dodoma
P.O.Box 43
DODOMA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NKANDI MADUHU BUZA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISH FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 593 ASQ. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI**
**KAH /RB/ 479 /2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE KAJUNA KAISHOZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI-ESCUDO** yenye namba za usajili **T222 CQR** chasis namba **TAQ1923210,** engine namba **G16A437002,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa
**DAR/OST/RB/286518/2022**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SULTAN SAIMON NZOYA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 189 DWA .**
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
**KAH /RB/ 486/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA LEMBENI**
**WILAYA YA MWANGA**
**KITUO CHA LEMBENI**
**MKOA WA KILIMANJARO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......05/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MGALLAH KIKO MGALLAH WA KIVERENGE MBUYUNI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA ZABIHUNA ALLY MGHAMBA**

### TANGAZO

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 03 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa tarehe 04 mwezi 07 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA**

**WILAYA YA MJINI TANGA KITUO CHA MJINI TANGA MKOA WA TANGA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA...149../2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: KUDURA ALLY MWINJUMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: MWANAUWANI MOHAMEDI KIKASHA**

### TANGAZO

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 26/07/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 19/07/2022

**HAKIMU**

---

MM AUCTIONEERS & DEBT COLLECTORS CO.LTD
Court Broker

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu Benki ya KCB tutauza kwa mnada wa hadhara mali/dhamana ya mdaiwa wa Benki, kama ilivyoorodheshwa hapo chini,mnada utafanyika kama ifuatavyo:-

1. NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 1253/28, KITALU 'C', C.T NO 131999, LO NO. 487762, MTONI KIJICHI MANISPAA YA TEMEKE, MALI YA ANDREW MHOJA MAZIKU AMBAYE NI MDHAMINI WA UNCTION TRADING COMPANY LIMITED, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 12/08/2022 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI
2. NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 2443, KITALU 'A', C.T NO 151737, LO NO. 630967, PUGU KAJIUNGENI MANISPAA YA ILALA , MALI YA UNCTION TRADING COMPANY LIMITED, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 13/08/2022 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI
3. NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA. 68, KITALU 'B', C.T NO 135338, LO NO. 551671, CHAMAZI MANISPAA YA TEMEKE, MALI YA NASSORO ALLY MSANGI, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 5/08/2022 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI

**MASHARTI YA MNADA**
1. Mnunuzi anatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na salio la asilimia 75% anatakiwa kulipa ndani ya siku kumi na nne (14)kuanzia siku ya mnada.
2. Mnunuzi akishindwa kulipa salio la asilimia 75% ndani ya siku kumi na nne (14) atakuwa amepoteza haki zake zote pamoja na asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
3. Nyumba inaweza kukaguliwa kuanzia tarehe ya tangazo hili mpaka siku ya mnada.
4. Mnunuzi anatakiwa kusimamia mwenyewe zoezi la kubadili hati ya kumiliki/mali aliyonunua na kulipa kodi zote stahiki.
5. Nyumba/mali itauzwa mahali na kama ilivyo

Wote mnakaribishwa

**Kwa mawasiliano:**
**KCB BANK MM AUCTIONEERS & DEBT COLLECTORS CO. LTD,**
**HEAD OFFICE HARAMBEE PLAZA**
**S.L.P 20306, DAR ES SALAAM**
**P.O.BOX 804, DAR ES SALAAM**
**SIMU: 0755 404 801/ 0715 401 801**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mwokota chupa, chuma chakavu akatwa vidole

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKAZI wa Kalimani Manispaa ya Moshi, Zuberi Salmini (35) anayejishughulisha na kuokota chupa na chuma chakavu, amenusurika kifo baada ya kupigwa kwa shoti ya umeme, mikanda na kukatwa vidole vya mkono wa kushoto na vijana wa karakana wakimtuhumu kuiba betri ya gari.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba wanawashikilia watu watano ambao majina yao yamehifadhiwa.

Kamanda Maigwa alisema tukio hilo lilitokea Julai 16, mwaka huu, majira ya saa 1:25 asubuhi, eneo la Oysterbay kata ya Bondeni, walikopokea taarifa kutoka kwa Msuya, kuwa mdogo wake alijeruhiwa na kukatwa vidole na kumsababishia maumivu.

"Walimtuhumu kwa wizi na kujichukulia sheria kwa kumkata vidole, muhanga amelazwa hospitali ya Mawenzi, kidole kimoja kimekatwa kabisa na kingine madaktari walikirudishia. Watuhumiwa wako kituoni kwa hatua za kisheria, tusingewahi (polisi) kufika huyu mtu angekufa,"alisema Kamanda huyo.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Rasul Msuya, alisema juzi kuwa Julai 16, mwaka huu, majira ya saa 12:00 asubuhi, akiwa kwenye majukumu yake, alisikia kelele za mtu anapigwa na aliposogea alimkuta kijana huyo.

Msuya alisema alikuta Salmin amefungwa miguu huku amening'inizwa kichwa chini miguu juu, akichapwa kwa mikanda na shoti ya umeme na kumiminiwa kahawa ya moto mwilini.

Alisema wakiwa hapo alikuja polisi mmoja ambaye aliwazuia watu hao kumuua lakini kidole kimoja walikichukua watesaji na hatujui walikipeleka wapi.

Msuya alisema: "Namfahamu kijana huyu kwa muda mrefu alikuwa utingo wa magari ya Kahe-Moshi baadaye akawa anaokota vyuma chakavu na chupa ambavyo alikuwa anaviuza, sijui kama ni mwizi kama walivyokuwa wanasema."

# Watoto familia moja waliokufa kwa utata wazikwa bila wazazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMIA ya wananchi wa Kijiji cha Mswakini Chini, Monduli mkoani Arusha, wameshiriki maziko ya watoto wanne wa familia moja yaliyofanyika nyumbani kwao, wanaodaiwa kuwa chanzo cha vifo vyao ni chakula chenye sumu walichokula.

Kutokana na utata wa vifo vya watoto hao, wazazi wa familia hiyo wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano zaidi juu ya chanzo cha vifo hivyo.

Awali, akiaga miili ya marehemu katika viwanja vya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, alisema wazazi wa watoto hao, walikaa nao kwa muda wa siku tatu kabla ya kuwapeleka hospitali hivyo kulikuwa na taarifa za kuzificha juu ya tukio hilo.

Hata hivyo, alisema Julai Mosi, mwaka huu, mtoto mkubwa, Bosii Nyangusi, baada ya kunywa maziwa ambayo hayajulikani yametoka wapi, alianza kuumwa na walimchukua na kumpeleka Babati na Hospitali ya FAME iliyoko wilayani Karatu, kwa ajili ya matibabu .

Mkuu huyo wa Wilaya, alisema Bosii baada ya hali yake kuwa mbaya. Julai 5 alifariki dunia na kuzikwa siku iliyofuata.

Mwaisumbe alisema vyombo vya usalama vilibaini kuna tatizo kwa kuwa kulikuwa na ufichaji wa taarifa hatimaye watoto hao kupoteza maisha.

Alisema uchunguzi uliofaywa awali na mtaalamu wa afya, umebaini kuwa kuna alama zinazoashiria watoto hao walikula kitu kibaya chakula au kinywaji kisichokuwa salama.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema mtaalamu huyo, alichukua sampuli kwa ajili ya kupeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya vipimo hivyo na vitatoka ndani ya wiki mbili zijazo na kama kuna mtu alihusika na vifo vya watoto hao watano watachukuliwa hatua za kisheria.

"Sampuli zimepelekwa Dodoma kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na baada ya wiki mbili zijazo majibu yatatolewa ili kama kuna waliohusika watachukuliwa hatua kali za kisheria," alisema.

Katika hatua nyingine, Mwaisumbe, ameitaka jamii ya kifugaji kuacha tabia ya kutumia dawa za miti shamba ambazo hazijathibitishwa na Wizara ya Afya na kutambuliwa kisheria.

Baba mdogo wa watoto hao, Loshilu Mollel, mkazi wa Kijiji cha Mswakini Chini, akizungumzia tukio hilo, alisema awali watoto hao walipoanza kuugua, alipigiwa simu kujulishwa na baba wa marehemu hao, Nyangusi Mollel.

Aliwataja marehemu hao ni Bosii Nyangusi (14) mwanafunzi wa darasa la sita shule ya msingi Mswakini (14), Veronica Nyangusi (10) darasa la tatu,Sofia Nyangusi (miaka sita) na mapacha wawili ambao ni Lenendoye (miaka minane) na Lemali Nyangusi (miaka minane)wanaosoma darasa la awali mswakini

Mollel alisema Julai 2, mwaka huu, Bosii alianza kuugua na kupatiwa dawa ingawa hakusema ni dawa gani katika duka la dawa baridi lililoko eneo la Kibaoni (Monduli).

Alisema kadiri siku zilivyosonga alijulishwa kuwa amezidiwa kwa kuwa alikuwa amevimba tumbo na walimkimbiza Fame, alipelekwa na baba yake mzazi na jirani yao mmoja.

Pia alisema Sophia na wenzake hali zao ziliziidi kuwa mbaya kwa kuwa walikuwa wamevimba matumbo na walipokuwa wakipewa chakula (uji na maziwa) walitapika.

Kadhalika alisema wakati wakiendelea kuwahudumia watoto hao wanne, walipokea taarifa kuwa Bosii amefariki kwa kuwa hali yake ilikuwa mbaya.




Mkuu wa Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe (mwenye miwani), akizungumza wakati wa kuaga miili ya watoto watano wa familia moja ya Kijiji cha Mswakini Chini, wanaodaiwa kupoteza maisha kwa kunywa maziwa yenye sumu, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Mahakama Kuu Ardhi yapiga hatua usikilizaji wa mashauri

**Na Munir Shemweta**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Ardhi imepiga hatua kubwa ya usikilizaji mashauri ya ardhi katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Julai, mwaka huu, na kupunguza mlundikano wa mashauri uliokuwapo awali.

Ulinganishaji kiwango cha ukamilishaji mashauri unaonyesha kuwa mahakama imeboresha kasi ya kusikiliza mashauri na kuwa na mashauri 1,591 yaliyosikilizwa kuanzia Januari, mwaka jana sawa na asilimia 42 ya mashauri yanayoendelea kusikilizwa hadi kufikia mashauri 1,212 sawa na asilimia 48 ya mashauri yaliyopo katika hatua ya kusikilizwa.

Mwelekeo unaonyesha kuwa pamoja na kasi inayoendela ya usikilizwaji mashauri, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi itabakiza asilimia 15 ya kesi ambazo hazijasikilizwa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Mahakama Kuu Dvisheni ya Ardhi imepunguza mlundikano wa mashauri ya ardhi yaliyofunguliwa kuanzia Julai, 2021 hadi Julai, 2022. Kwa Julai 2021 kulikuwa na mashauri 359 yaliyosikilizwa," alisema Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, Agnes Mgeyekwa.

Aidha, takwimu zinaonesha mlundikano wa mashauri ya ardhi umeendelea kupungua siku hadi siku kutokana na maboresho mbalimbali yanayoendelea kufanywa na Mahakama Kuu ikiwemo matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

"Matumizi ya TEHAMA yamesaidia sana utendaji kazi wa mahakama yetu ikiwamo uwasilishwaji mashauri. Wanaoshitakiana sasa hawalazimiki kufika kwenye majengo ya mahakama," alisema Mgeyekwa.

Kwa mujibu wa Jaji Mgeyekwa, katika kuunga mkono azma ya mahakama kuelekea mahakama mtandao, divisheni yake inafanya kazi nyingi kwa kutumia TEHAMA ikiwamo kusikiliza baadhi ya mashauri kwa njia ya mikutano (video conference).

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Jaji Mgeyekwa aliongeza kuwa mahakama hiyo kwa sasa iko kwenye mabadiliko ya kuelekea mfumo wa kidigitali utakaoiwezesha kuunganishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kutambua hatimiliki za Ardhi.

Jaji Mgeyekwa alisema pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa katika kuboresha utendaji kazi wa Mahakama Kuu - Divisheni ya Ardhi, bado kuna changamoto kadhaa alizozieleza kuwa iwapo zitapatiwa ufumbuzi haraka divisheni hiyo inaweza kufanya vizuri zaidi kuliko inavyofanya sasa.

Hivi karibuni, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, alifanya ziara katika Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi na katika ziara yake hiyo alisema umefikia wakati taarifa zinazokusanywa na wizara husika zipatikane kwa wananchi ili masuala ya ardhi yawe wazi zaidi na yasiibue migogoro ambayo inachukua muda mrefu mahakamani.

Aidha, Jaji Mkuu alibainisha juu ya umuhimu wa Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi kuangalia pia uwezekano wa kutumia usuluhishi kama njia mojawapo ya kupunguza mlundikano wa mashauri ya ardhi.

# TAMISEMI DODOMA MABINGWA WAPYA KLABU BINGWA NETIBOLI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Tamisemi kutoka Dodoma imekabidhiwa zawadi ya Sh. milioni mbili baada ya kuibuka vinara katika Klabu Bingwa ya Netiboli Ligi Daraja la Kwanza iliyomalizika kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

Tamisemi wametwaa ubingwa huo kwa kufikisha pointi 16 na kuwavua wapinzani wao, JKT Mbweni ya Dar es Salaam waliokuwa wanalishikilia kombe hilo kwa miaka mitatu mfululizo ambao wamemaliza katika nafasi ya pili wakiwa na pointi 14.

Mbali na fedha, mabingwa walikabidhiwa kikombe na medali za dhahabu kutoka katika Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA).

Akizungumza baada ya mchezo wa mwisho kumalizika, Kocha Mkuu Tamisemi, Maimuna Kite, alisema ameshukuru timu yake kutwaa ubingwa huo baada ya kukaa muda mrefu bila kombe.

> **"Siri ya ushindi wa leo ni maandalizi ya muda mrefu tuliyoyafanya pamoja na utimamu wa mwili waliokuwa nao wachezaji wangu, wali kuwa pia na nidhamu ya kimchezo," alisema Kitete.**

Kocha huyo alisema ligi hiyo ilikuwa ngumu na mpinzani wake alishindwa kupata nafasi ya kumfunga kwa sababu alijipanga imara kumdhibiti katika kila idara.

Alisema anaishukuru Ofisi ya Rais kwa sapoti kubwa waliyoipata katika kipindi chote cha maandalizi ya ligi hiyo na kuongeza waliahidi kurejea Dodoma na ushindi.

Alisema baada ya ushindi huo kwa sasa wanakwenda kujipanga vyema ili kujiandaa na Ligi ya Muungano ambayo itafanyika Oktoba, mwaka huu.

Naye mgeni rasmi, Gilbert Kaijage ambaye aliwapongeza mabingwa hao wapya kwa kupambana na hatimaye kutimiza malengo yao.

Kaijage alisema atashirikiana na CHANETA kuhakikisha wanakuwa na viwanja vyenye ubora pamoja na makocha wenye sifa kutoka nje ya nchi.

"Tutashirikiana pamoja na Chaneta kuhakikisha wanakuwa na miundombinu mizuri pamoja na kufanya jitihada za kutafuta walimu wa nje ya nchi ili waje kuuendeleza zaidi mchezo huu," alisema Kaijage.

Ligi hiyo ilishirikisha timu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa CHANETA, Rose Mkisi, alisema timu zilizoshindwa kushiriki ligi hiyo bila ya kutoa taarifa rasmi zimeshushwa daraja na kuongeza msimu ujao Klabu Bingwa Daraja la Kwanza itashirikisha timu 12.



Wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya kucheza ngoma kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya UMISETA itakayofanyika mwezi ujao mkoani Tabora. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam yaelekea Misri na Nado*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI winga machachari wa Azam FC, Idd Selemani 'Nado' anatarajiwa kuanza mazoezi mwezi ujao baada ya kuwa nje kwa kiasi cha miezi tisa, kikosi cha timu hiyo kitaondoka nchini kesho kuelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na msimu mpya.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia maarufu kama 'Zaka Zakazi' alisema jana tayari Nado ameshapona na atakuwa mmoja wa wachezaji watakaoondoka kwenda katika Mji wa El Gouna kuweka kambi.

"Uzuri ni kwamba Nado hajadanganya umri, ndiyo maana matibabu yake yameenda vizuri na sasa amepona. Amekuwa nje kwa muda wa miezi tisa, madaktari wameshauri mwezi ujao aanze mazoezi mepesi. Na niwaambie ni mmoja wa wachezaji tutakaokwenda nao kambini, sidhani kama ataanza kwenye mechi za kwanza za ligi kwa sababu hajacheza muda mrefu, anahitaji kukaa zaidi na kuwa fiti," alisema Zaka.

Kuhusu safari ya kambi, Zaka alisema baadhi ya wachezaji waliowasajili wataungana na kikosi hicho Misri.

"Sisi tumeshaanza mazoezi, siyo kama tukienda huko ndiyo tunaanza, hapana, tumeanza nyumbani tunapokwenda huko tunaenda kuendeleza. Huku tayari watu wameshatoa mafuta kwa sababu wametoka kwenye bata, huko tunaenda kuendelezea tulipoishia," Zaka alisema.

## Mafunzo yatema nyota wake tisa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Mafunzo FC umetangaza kuwaacha wachezaji wake tisa waliokuwa nao katika msimu uliomalizika na umeanza mikakati kujiimarisha kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2022/2023, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Mafunzo FC, Abdullah Bakari "Edo" alisema sababu kubwa ya kuwaacha wachezaji hao ni kushuka viwango na watatumia nafasi hizo kusajili wengine watakaokabiliana na ugumu wa Ligi Kuu Zanzibar wanayoshiriki.

Edo alisema mabosi wa Mafunzo na wachezaji hao wamefikia makubaliano na wametangaza mapema ili kuwapa nafasi ya kwenda kusajiliwa na timu nyingine.

"Wachezaji tuliowaacha wapo ambao tumekaa naona katika timu takribani miaka mitatu na wengine miaka miwili, sio kama hawajui hapana wengine viwango vyao kidogo vimeshuka lakini wengine walikuwa hawapati namba katika kikosi chetu, hivyo tukaona ni vyema tuwape nafasi wakajaribu kwingine," Edo alisema.

Alisema kikosi chake ambacho msimu uliopita kilimaliza katika nafasi ya tatu kimeshaanza mazoezi kwa ajili ya msimu mpya.

## Asukile atangaza kustaafia Prisons

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Tanzania Prisons, Benjamin Asukile, amesema licha ya mkataba wake kukaribia ukingoni, lakini hafikirii kuhama kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo na klabu hiyo.

Asukile ambaye amekuwa chachu ya timu hiyo kubaki katika Ligi Kuu msimu huu, akifunga mabao muhimu katika mechi za mwisho zilizoifanya kutoka mkiani na kwenda kwenye mchujo, ameweka wazi ataendelea kubakiwa Prisons licha ya kupokea ofa kutoka klabu mbalimbali.

"Kusema kweli msimu ulikuwa mgumu na ushindani wa hali ya juu, nashukuru tumebaki na nitaendelea kuwapo kwenye klabu hii. Wengi hawajui mimi niliwahi kuondoka hapa, niliingia Prisons 2009, mwaka mmoja baadaye nikahamia Kagera Sugar, nikacheza hadi 2015, nikarudi tena hapa 2016 hadi leo hii, nitaendelea kuwa hapa kwa sababu ni klabu ninayoipenda na ipo moyoni mwangu," alisema Asukile.

Hata hivyo, kuna taarifa kuwa kutokana na mchango wake mkubwa alioutoa kwa timu hiyo, huenda akapata ajira rasmi kwani timu hiyo inamilikiwa na Jeshi la Magereza Tanzania.

## ZISIKUPITE

### CITY ILIMKATAA NEYMAR

KLABU ya Paris St-Germain ilikuwa tayari kumtoa mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 30 kwa Manchester City ili kubadilishana na kiungo wao wa kati, Bernardo Silva (27), lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England walikataa mpango huo. ***(Le Parisien)***

### LIVERPOOL YAMTAKA ANTONY

LIVERPOOL wameulizia kuhusu kumsajili winga wa Ajax, raia wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Manchester United. ***(Football Insider)***

### KOUNDE AKARIBIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inakaribia kufikia makubaliano na Sevilla kwa kitita cha pauni milioni 60 kumnunua mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde lakini huenda wakakabiliana na ushindani kutoka kwa Barcelona kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Guardian)***

### KIMPEMBE ATAJWA EPL

CHELSEA pia ipo katika mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu mkataba wa pauni milioni 50 kwa Presnel Kimpembe, lakini wanahofia beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26 atakataa kuhamia Stamford Bridge. ***(Standard)***

### LEWANDOWSKI NA BARCA

BARCELONA wamemsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich kwa mkataba wa miaka minne wenye thamani ya euro milioni 50.***(Bild)***

### ZANIOLO ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 23 kutoka AS Roma, lakini wanahitaji kuwauza baadhi ya wachezaji kwanza ili kufanikisha mchakato huo. ***(Calciomercato)***

### WINKS KUONDOKA SPURS

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya England, Harry Winks mwenye umri wa miaka 26 na winga wa Hispania, Bryan Gil (21) ni miongoni mwa wachezaji wanane wa kikosi cha kwanza cha Tottenham Hotspur ambao wameambiwa wanaweza kuondoka msimu huu wa joto. ***(Standard)***

### LINGARD ANUKIA FOREST

KLABUya Nottingham Forest ndio timu ya hivi karibuni zaidi kuonyesha nia ya kumnunua winga wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, ambaye pia amefanya mazungumzo mapya na West Ham. ***(Guardian)***

### CUCURELLA AWEKWA SOKONI

KLABU ya Brighton itadai zaidi ya pauni milioni 50 kutoka kwa Manchester City ili kumnunua beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 23. ***(90Min)***

### AZPILICUETA NJIA MOJA

CHELSEA wako tayari kumruhusu mlinzi wa Timu ya Taifa ya Hispania, Cesar Azpilicueta kuondoka kwenda Barcelona mara tu watakapopata mbadala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA AELEZEA USAJILI WA NEYMAR

**MANCHESTER,** England

●●● Kocha huyo asema alikataa pendekezo la kubadilishana na Bernardo kwa sababu...

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekana uvumi unaowahusisha mabingwa hao wa Ligi Kuu England na mpango wa kutaka kumsajili Neymar kutoka Paris Saint-Germain.

**Gazeti la Ufaransa la Le Parisien liliripoti PSG watamtoa Neymar kwa City kama sehemu ya mpango wa kubadilishana na Bernardo Silva.**

Kwa mujibu wa Daily Mail, City ilikataa pendekezo hilo, lakini Guardiola alifafanua habari hiyo haikuwa sahihi.

"Pole sana kwa Le Parisien, lakini si kweli," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari mjini Houston nchini Marekani kabla ya mchezo wao wa kujiandaa na msimu dhidi ya Club America, hapo jana.

"Nawapa pole kwa sababu taarifa walizozipata ni za uongo.

"Neymar ni mchezaji wa aina yake na kwa taarifa yangu, ni mtu mzuri. Acha ajielezee akiwa Paris.

Imeripotiwa msimu huu PSG wamemweka sokoni Neymar mwenye umri wa miaka 30, huku Guardiola akisisitiza imani yake, Bernardo atabakia City licha ya hapo awali kuhusishwa na Barcelona.

City wamenunua wachezaji kadhaa muhimu msimu huu, Erling Haaland, Kalvin Phillips, Julian Alvarez na Stefan Ortega Moreno, wakati Bernardo amejiimarisha kuwa mchezaji muhimu katika safu ya kiungo.

Mabingwa hao wa England walishinda mbio za kumpata fowadi wa Norway Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund, huku matarajio yake yakiwa makubwa katika klabu ambayo ilionekana kukosa mshambuliaji msimu uliopita.

"Hatuwezi kuweka shinikizo kubwa kwa wachezaji hawa," alisema Guardiola.

Guardiola pia hakufunga mlango wa kusajili zaidi, huku wachezaji kama Raheem Sterling, Gabriel Jesus na Oleksandr Zinchenko - ambaye anatarajiwa kujiunga na Arsenal - wote wameondoka.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,016,4

MECHI KALI
RB LEIPZIG
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 3.05
X | 3.64
2 | 2.01

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE LIGT KUISAIDIA BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

MLINZI Matthijs de Ligt kuondoka Juventus kwenda Bayern Munich ni "ishara nzuri" kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa mujibu wa kocha, Julian Nagelsmann.

Beki huyo wa kati alijiunga na Bayern kwa mkataba wa thamani ya euro milioni 80 na alisaini mkataba wa miaka mitano Jumatatu, na hivyo kuhitimisha muda wake wa miaka mitatu kule Turin.

De Ligt amekuwa mchezaji wa nne kuwasili katika dirisha hili la uhamisho wa Bayern Munich baada ya kuongezwa kwa Sadio Mane na wachezaji wawili wa Ajax, Noussair Mazraoui na Ryan Gravenberch.

Bayern wameripotiwa kuwashinda Chelsea na Manchester United waliomtaka De Ligt, ambaye alichezea Juve kwa dakika 2,675.

"Nina furaha sana kwamba tumempata. Bado ni mchanga sana na tayari ana kazi nzuri," alisema Nagelsmann.

"Ni ishara nzuri kwetu na kwa Bundesliga nzima kwamba tumempata. Ni kiongozi na anaweza kufanya mambo mengine, akiwashauri wachezaji. Natumaini anaweza kuwafahamu wachezaji wenzake hivi karibuni."



## Lewandowski apewa mi4 Barca

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imethibitisha makubaliano ya mwisho ya kumsajili, Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich kwa euro milioni 50, pamoja na nyongeza, kwa mkataba wa miaka minne.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland alisafiri hadi Miami nchini Marekani kukutana na wachezaji wenzake wapya Jumapili, siku moja baada ya Barca kuthibitisha wamefikia makubaliano ya kimsingi na Bayern Munich.

Lewandowski baadaye alifuzu vipimo vyake vya afya, huku Bayern Munich "rasmi" wakitangaza wamemuuza.

Barca hivi karibuni ilithibitisha taarifa za uhamisho wa mshambuliaji huyo mwenye mvuto, ambaye atakuwa na kipengele cha kumnunua cha euro milioni 500.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alifunga mabao 50 katika michuano yote msimu uliopita, mabao mengi zaidi katika ligi tano bora za Ulaya, Bayern Munich iliponyanyua taji lao la 10 la Bundesliga.

Mabao 312 ya mshambuliaji huyo wa Bundesliga ni ya pili kwa mchezaji yeyote katika historia ya mashindano hayo, nyuma ya Muller (365), huku akiacha Bayern amejikusanyia mabao 344 na asisti 57 katika mechi 375 katika mashindano yote.

28,582/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/07/22 | 19:15 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 02. 23/07/22 | 21:30 | Hannover vs St. Pauli | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 03. 23/07/22 | 21:30 | Sarmiento vs Colon Santa Fe | 2.42 | 3.14 | 3.14 |
| 04. 23/07/22 | 22:30 | Vila Nova GO vs Vasco da Gama | 2.63 | 2.73 | 3.08 |
| 05. 24/07/22 | 00:30 | Nautico PE vs Londrina PR | 2.30 | 2.97 | 3.36 |
| 06. 24/07/22 | 02:30 | CRB AL vs Novorizontino SP | 2.48 | 2.93 | 3.08 |
| 07. 24/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs Nashville | 2.32 | 3.42 | 3.02 |
| 08. 24/07/22 | 02:30 | Orlando City vs Philadelphia Union | 2.37 | 3.43 | 2.93 |
| 09. 24/07/22 | 03:00 | Botafogo RJ vs Atletico Pr | 2.30 | 3.33 | 3.03 |
| 10. 24/07/22 | 03:00 | DC United vs Montreal Impact | 2.31 | 3.38 | 3.07 |
| 11. 24/07/22 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Los Angeles FC | 2.90 | 3.50 | 2.35 |
| 12. 24/07/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs Chicago Fire | 2.28 | 3.45 | 3.05 |
| 13. 24/07/22 | 12:00 | Tokyo Verdy vs Yokohama | 2.90 | 3.30 | 2.42 |
| 14. 24/07/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 15. 24/07/22 | 17:00 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.55 | 3.40 | 2.65 |
| 16. 24/07/22 | 22:00 | Westerlo vs Cercle Brugge | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 17. 24/07/22 | 22:00 | Juventude RS vs Ceara CE | 2.58 | 2.98 | 2.93 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 21/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 2622 | FK Liepaja vs BSC Young Boys | 14.14 | 6.87 | 1.17 |
| 17:00 | 5455 | Kairat Almaty vs Kisvarda FC | 2.12 | 3.29 | 3.39 |
| 17:00 | 5463 | Tobol Kostanay vs Lincoln FC | 1.35 | 4.66 | 8.91 |
| 18:00 | 3325 | Valmiera Fk/Bjss vs Shkendija | 2.10 | 3.28 | 3.48 |
| 18:00 | 5269 | Ararat Armenia vs Paide Linnameeskond | 1.63 | 3.79 | 5.25 |
| 18:30 | 2047 | Danubio FC vs Plaza Colonia CD | 2.19 | 3.08 | 3.13 |
| 18:30 | 5961 | Makedonija GjP vs CSKA Sofia | 4.22 | 3.52 | 1.82 |
| 19:00 | 2359 | Seinajoen JK vs Lillestrom | 4.53 | 3.63 | 1.74 |
| 19:00 | 2461 | Zira vs Maccabi Tel Aviv | 3.93 | 3.38 | 1.93 |
| 19:00 | 2581 | Lech Poznan vs Dinamo Batumi | 1.79 | 3.64 | 4.24 |
| 19:00 | 3438 | Luka Koper vs FC Vaduz | 1.75 | 3.59 | 4.55 |
| 19:00 | 4711 | Saburtalo Tbilisi vs Steaua Bucuresti | 5.25 | 3.79 | 1.63 |
| 19:00 | 5081 | Molde vs Elfsborg | 1.89 | 3.68 | 3.73 |
| 19:00 | 5189 | KuPS Kuopio vs Milsami Orhei | 1.26 | 5.43 | 11.06 |
| 19:30 | 1882 | Pogon Szczecin vs Brondby | 1.92 | 3.43 | 3.89 |
| 19:30 | 3903 | Ruzomberok vs FC Riga | 2.24 | 3.13 | 3.28 |
| 19:30 | 3909 | Eastern Company SC vs El Ittihad Alexandria | 3.81 | 3.06 | 2.06 |
| 19:30 | 4082 | Suduva vs Viborg FF | 5.03 | 3.67 | 1.67 |
| 20:00 | 1097 | Royal Antwerp vs KF Drita | 1.17 | 6.66 | 15.14 |
| 20:00 | 1265 | Levski Sofia vs PAOK | 3.47 | 3.17 | 2.14 |
| 20:00 | 2012 | Vorskla Poltava vs AIK Football | 6.07 | 3.79 | 1.56 |
| 20:00 | 2558 | FC Basel vs Crusaders Belfast | 1.10 | 8.30 | 23.28 |
| 20:00 | 2715 | ST Josephs FC vs Slavia Prague | 28.28 | 8.48 | 1.09 |
| 20:00 | 3326 | B36 Torshavn vs SP Tre Fiori | 1.24 | 5.83 | 11.06 |
| 20:00 | 3521 | Rapid Vienna vs Lechia Gdansk | 1.68 | 3.83 | 4.64 |
| 20:00 | 3664 | Sparta Prague vs Viking | 1.55 | 4.15 | 5.46 |
| 20:00 | 5141 | Videoton FC vs Gabala | 1.31 | 4.94 | 9.49 |
| 20:15 | 4693 | RB Leipzig vs Liverpool | 3.05 | 3.64 | 2.01 |
| 20:30 | 5435 | Aris Limassol vs Neftchi Baku | 2.34 | 3.16 | 3.06 |
| 20:30 | 5606 | CFR Cluj vs Inter Club De Escaldes | 1.08 | 9.08 | 30.25 |
| 20:30 | 5992 | Hapoel Beer Sheva vs Dinamo Minsk | 1.72 | 3.67 | 4.63 |
| 20:45 | 3530 | Basaksehir vs Maccabi Netanya | 1.46 | 4.16 | 6.90 |
| 21:00 | 2898 | Aris Salonica vs Gomel | 1.17 | 6.44 | 17.11 |
| 21:00 | 4317 | RFCU Luxembourg vs Cukaricki St | 5.46 | 3.84 | 1.60 |
| 21:00 | 4487 | River Plate (URU) vs Defensor Sporting | 2.55 | 3.18 | 2.55 |
| 21:00 | 5753 | Sepsi Osk vs Olimpija Ljubljana | 1.71 | 3.64 | 4.75 |
| 21:30 | 1209 | Velez Mostar vs Hamrun Spartans | 1.66 | 3.79 | 4.95 |
| 21:30 | 3034 | HNK Rijeka vs Djurgardens IF | 2.39 | 3.23 | 2.93 |
| 21:30 | 4612 | Spartak Trnava vs Newtown AFC | 1.16 | 6.66 | 17.16 |
| 21:30 | 4985 | AZ Alkmaar vs FK Sloga Simin Han | 1.11 | 8.25 | 22.13 |
| 21:45 | 2505 | Motherwell vs Sligo Rovers | 1.44 | 4.34 | 6.86 |
| 21:45 | 5427 | St Patricks vs NK Mura | 2.50 | 3.23 | 2.78 |
| 22:00 | 3152 | BATE Borisov vs Konyaspor | 4.84 | 3.98 | 1.63 |
| 22:00 | 4748 | Al Ahly Cairo vs Zamalek | 2.14 | 2.85 | 3.54 |
| 22:00 | 5281 | Rakow Czestochowa vs Astana | 1.66 | 3.70 | 5.06 |
| 22:00 | 5597 | Vllaznia vs Universitatea Craiova | 4.24 | 3.48 | 1.83 |
| 22:15 | 5448 | Breidablik vs Buducnost | 1.90 | 3.54 | 3.84 |
| 22:30 | 3261 | Rosario Central vs NewellS Old Boys | 2.54 | 2.93 | 2.74 |
| 22:30 | 4326 | Vikingur Reykjavik vs The New Saints | 1.60 | 3.94 | 5.26 |
| 22:30 | 5152 | Vitoria Guimaraes vs Puskas Akademia | 1.46 | 4.26 | 6.69 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KOCHA AZAM ATAMANI KUIVAA SIMBA SC MISRI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdulhamid Moallin, anatamani kupata mechi ya kirafiki dhidi ya Simba kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 pamoja na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki.

**Azam FC wanatarajia kuondoka nchini kesho kuelekea Misri ambapo Simba pia ipo huko ikijiandaa na msimu mpya.**

Moallin aliliambia gazeti hili baada ya mapumziko mafupi sasa, wamerejea mazoezini na watakuwa na programu mbili za mazoezi.

Kocha huyo alisema, jambo la msingi wanataka kutengeneza mfumo mpya wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao kwa kuwapa mambo mbalimbali ya kiufundi.

"Tutakuwa na michezo ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao, kubwa ni kutengeneza muunganiko wa wachezaji ili kufikia malengo tulioyojiwekea," alisema kocha huyo.

Alisema kuhusu safari yao ya Misri wameamua kwenda huko kwa sababu watapata utulivu wa kutekeleza kikamilifu programu za mazoezi na kurejea nchini wakiwa imara na tayari kushiriki Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.

"Nafikiri ni wakati wa kukamilisha michezo ya kirafiki tukiwa Misri katika kambi hii ya maandalizi ya msimu mpya, tunapaswa kucheza michezo mingi ya kirafiki tukiwa nchini humo, natambua kutakuwa na timu mbili kutoka Tanzania nchini humo, sisi Azam FC lakini pamoja na Simba," alisema kocha huyo.

Azam FC ilimaliza msimu uliopita ikiwa katika nafasi ya tatu huku ikitolewa na Coastal Union kwenye mechi ya mashindano ya Kombe la FA.



Mkufunzi wa Waamuzi wa Soka wa Kimataifa, Leslie Liunda (kulia), akitoa maelekezo katika semina ya waamuzi wanaochezesha Ligi ya Championship na First League kutoka mikoa mbalimbali inayofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Coastal Union kucheza usiku*



**Na Cheji Bakari,** TANGA

UWANJA wa CCM Mkwakwani utaanza kutumika usiku katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2022/2023 imeelezwa.

Meneja wa uwanja huo, Nassoro Makau alisema ufungaji wa taa unafanyika kutokana na makubaliano kati ya Kampuni ya Azam Media na uongozi wa uwanja na mchakato utaanza mapema wiki ijayo.

"Ufungaji wa taa katika uwanja huu ni mradi wa Azam Media ambao kwa mujibu wa mkataba wao wana asilimia 75 na sisi, uongozi wa uwanja wa Mkwakwani tuna asilimia 25, lengo ni kuupa uwezo uwanja uweze pia kuchezwa mechi za usiku," alisema Makau.

Aliongeza mbali na ufungaji wa taa hizo, pia wanaendelea na ukarabati mwingine mdogo katika maeneo muhimu matatu.

" Sisi wenyewe sasa hivi tunaendelea na ukarabati katika eneo la kuchezea, vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji na eneo la benchi la ufundi," alisema meneja huyo.

Kuhusu Sh. bilioni 10 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kukarabati viwanja vitano kikiwamo, CCM Mkwakwani, alisema bado mwongozo kwa kinachofanyika sasa ni sehemu ya bajeti ya kila mwaka inayotengwa na uongozi wa uwanja kurekebisha maeneo yenye changamoto.

Michezo
Alhamisi Julai 21, 2022
Nipashe



Guardiola aelezea usajili wa Neymar UKURASA 21




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa (katikati), akikabidhi bendera ya Taifa kwa wanariadha wanaotarajia kwenda Uingereza kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Usajili wa Manzoki waikamua Simba

**Na Saada Akida**

## ●●● Yavunja mkataba wake Vipers, Kagere, Mugalu, Lwanga 'out'...

KATIKA kuhakikisha inatimiza mipango yake, uongozi wa Simba ya jijini Dar es Salaam umeonyesha jeuri ya fedha baada ya kutoa Sh. milioni 100 ili kuvunja mkataba wa straika wa Vipers ya Uganda, Cezar Manzoki, imefahamika.

**Manzoki amekuwa kwenye rada za Simba kwa muda mrefu na taarifa zilizopatikana jijini zinasema Wekundu wa Msimbazi walishamalizana na straika huyo lakini kikwazo kilikuwa ni mkataba wake na Vipers uliokuwa unamalizika Oktoba, mwaka huu.**

Taarifa zaidi zinasema Manzoki ataungana na kikosi cha Wekundu wa Msimbazi wakati wowote kuanzia sasa baada ya viongozi wa klabu hiyo kufikia uamuzi wa kulipa fedha walizotakiwa za kuvunja mkataba.

Chanzo hicho kilisema tayari wameshafuata taratibu zote za usajili na nyota huyo wameingia naye mkataba wa miaka miwili .

"Baada ya kuona hali hiyo tulimteua mjumbe mmoja akaenda Uganda kulipa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya mchezaji huyo kuwa huru ili aweze kujiunga rasmi na klabu yake mpya ya Simba, lakini pia kupata kibali (ITC) cha kumruhusu kucheza."

"Manzoki ni miongoni mwa wachezaji watatu wapya ambao bado hawajatambulisha akiwamo Nelson Okwa pamoja na Mohammed Ouattara ambao muda wowote kuanzia sasa watatambulishwa na kujiunga na timu hiyo nchini Misri kuendelea na Pre Season," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza ujio wa nyota huyo utafanya idadi ya wachezaji wa kigeni kuwa kubwa na kwa maana hiyo imewalazimu mabosi wa Simba kufanya mazungumzo na kufikia makubaliano ya pande zote mbili ya kuvunja mikataba na nyota wake watatu.

"Usajili wa wachezaji hao itatulazimu kupunguza nyota watatu wa kigeni tuliokuwa nao, tuko katika makubaliano ya kuvunja mikataba na wachezaji watatu ambao ni Meddie Kagere, Chriss Mugalu pamoja na Thadeo Lwanga," .

"Kagere na Mugalu wana mkataba wa mwaka mmoja kila mmoja na Lwanga bado ana mkataba wa miaka miwili, tuko kwenye makubaliano ya kulipwa stahiki zao na nafasi hizo kuchukuliwa na wachezaji hao watatu wapya ambao tutawatambulisha muda wowote," kiliongeza chanzo chetu.

Kuhusu suala la fedha kwa sasa Simba hawana shida kwa sababu ya kusaini mkataba mnono na mdhamini mpya ambaye ni Kampuni ya M-Bet.

Wakati huo huo, Simba imefikia makubaliano na kipa wake, Aishi Manula kwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu ambao utamalizika ifikapo mwaka 2025.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema wanaendelea kuimarisha kikosi chao ikiwamo kuwaongezea mikataba wachezaji ambao bado wanawahitaji na msaada mkubwa ndani ya klabu hiyo.

Alisema ushindani wa kuinasa saini ya Manula ulikuwa mkubwa baada ya mlinda mlango huyo kutakiwa na klabu mbalimbali za hapa nchini na nje ya Tanzania.

"Kwa kutambua umuhimu na ubora wa mlinda mlango huyo, klabu ikaamua kumwongezea mkataba wa muda mrefu zaidi, tunatambua ubora wa Manula ndani na nje ya mashindano ambayo Simba tumecheza," alisema Ahmed.

Alisema zoezi la utambulisho wa wachezaji wapya bado linaendelea kwa kushusha silaha mpya tatu ambazo wanaamini zitaimarisha kikosi chao.

# Nabi aitazama nidhamu Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema nidhamu na kujituma kwa kila wachezaji wake ndio kitu anachohitaji kukiona ambacho kitasaidia kutetea mataji waliyobeba msimu uliopita, lakini itawasaidia kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kikosi cha Yanga kinaingia kambini leo huku Nabi ambaye alikuwa kwao kwa mapumziko akitarajiwa kurejea nchini leo na kuelekea moja kwa moja Avic Town, Kigamboni ili kuanza rasmi maandalizi ya msimu mpya wa 2022/2023.

Nabi alilimbia gazeti hili usajili uliofanyika ni mzuri na kikubwa atasisitiza wachezaji wake kuonyesha nidhamu ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu atakayowapa.

Alisema wakiwa mapumziko, alitoa programu kwa wachezaji wake wa zamani na wapya waliosajiliwa ili kuanza mazoezi ya kuiandaa miili yao kuwa fiti na yenye utimamu.

"Msimu mpya hautakuwa rahisi kwa sababu ya usajili uliofanywa na timu nyingine, pia ukizingatia tunaenda kushiriki michuano ya CAF tunatakiwa kuwa imara na kufika hatua ya robo fainali, hatuwezi kufika huko lazima tuwe na hali ya nidhamu na kujituma katika kila mechi," alisema Nabi.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari wachezaji wa kigeni wameshawasili na kuingia kambini moja kwa moja tangu jana.

"Kocha amewataka wachezaji waingie kambini mapema bila kusubiri waliopo Timu ya Taifa, ana programu za wao pekee kabla ya wale waliopo katika majukumu ya mataifa yao," alisema Bumbuli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >